SportPesa
TZS. 918,137,180
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Wanafamilia wauawa madai wizi wa pikipiki**

UKURASA 3



BUFE
Ijumaa Februari 11, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Wakala mbegu wajitosa kuzalisha alizeti, michikichi kunusuru uhaba
kurasa 12

MZIGO HUU WA VITAMBULISHO NOMA SANA
Ukurasa 13

BIASHARA

**Mkufunzi NCT Dk. Divecha: Mhudumu hoteli silaha kuu milango 5 ya fahamu**

- Unadhifu, tabasamu, ukarimu, lugha kadhaa...
- Mgahawa wake balaa!...akampikia Rais Mwinyi
- Ugali aliopika Nairobi ukampa 'scholarship' nje

Na Christina Mwakangale

UMEWAHI kufikiri kwamba katika shughuli zako za kibiashara na zinazokuunganisha wewe pamoja na wateja kwamba, zinahusiana na milango ya fahamu?

Binadamu ana milango mitano ya fahamu; masikio, ulimi, macho, ngozi na pua, vikitajwa kuwa na uhusiano mkubwa na mbinu za kumteka mteja katika biashara.

Mkufunzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), Dk. Milan Divecha, anasema kati ya makosa yanayofanyika kwenye biashara ni kutoitumia milango hiyo ya fahamu, ambayo kila moja ina kazi yake.

Mwanazuoni huyo wa masuala ya hoteli zaidi ya miaka 30, anatoa siri ya kufanikiwa kufanya biashara hasa ya mapishi katika hoteli na migahawa, wakati wa kongamano la kuelekea mahafali ya 19 ya NCT, jijini Dar es Salaam, hivi karibuni.

Hapo wamehitimu wasomi wa mafunzo ya ukarimu, mapishi, uhudumu chakula na vinywaji, utunzaji vyumba, kufua, uongozi na usafirishaji watalii, uratibu matukio na mapokezi kwa ngazi ya astashahada na stashahada.

Dk. Divecha anasema mteja anapofika kwenye biashara, iwe hoteli au mgahawa, mtoa huduma usikilize kwa makini hapo nua:"Tumia sikio kusikia inapolia chakula kimeisha, ini au mteja ataongeza.

Mkufunzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), Dk. Milan Divecha. PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE

"Tumia tabasamu, tazama kila kitu alipo mteja wako sio unamtelekeza meza haina chochote au imepungua kitu fulani hadi aanze kukutafuta kukuita. Inaleta usumbufu na kesho asirudi, 'customer care' ni kitu kikubwa.

"Mteja anapofika hotelini kwako unatakiwa kumsikiliza kwa masikio yako. Tuna milango mitano ya fahamu, mitano ambayo inatumika katika 'customer service'. Kwenye utafiti tumebaini watu wanaangalia, lakini hawasikilizi wanayotakiwa kufanya.

"Kwa mwonekano (mhudumu) unaonekana kuvutia, unapendeza hata kufanya mazungumzo na mteja upo vizuri. Lakini, kumpokea mgeni unafahamu?," anahoji Divecha.

"Mteja amekuja kwenye hoteli yako, amekaa na kuagiza chakula? Unatakiwa kumsikiliza na kumpatia chakula muda muafaka na hakikisha kuna kila kitu kwenye meza aliyokaa. Sio mara chumvi imekosekana au haitoki, uma, kisu hakuna. Umempokea vizuri na chakula kapata ndani ya muda, je meza yako imekamilika?"

MGAHAWANI KWAKE

Anasimulia kilichojiri katika mgahawa wa kwanza alioanzisha mkoani Dar es Salaam, akisema: "Mgahawa niliouanzisha na kuwa na hadhi ya juu mtaa wa Samora (Alcove Restaurant) ilikuwa 'Project' yangu ya Masters'(Utafiti Shahada ya Uzamili). Nilifikiria kubadili aina ya shughuli za kifamilia, sababu, mtoto mhandisi mama mhasibu, fikiria ningewezaje.

"Nilipohitimu National Service (JKT) nilipata fursa ya kazi Nairobi (Kenya) kama 'entern'() mahali fulani, kwa sababu nilikuwa najua kupika chakula na kile nilichojifunza nikiwa shuleni, hasa kupika ugali, maharage, mchicha na nyama ya kuchoma nilijikita hapo hapo.

"Kule Nairobi kukiwa na kongamno au wakihitaji 'catering' walikuwa wakihitaji chakula na nilipika, wakaanza kuniulizia kwenye kila hafla. Chakula cha watu 25 nilimudu kukipika vizuri tu, hii ilinifanya kupata 'scholarship' Uswisi," anasema Dk.Divecha.

Inaendelea Uk.12

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Februari 11, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580853
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Magazeti maarufu yatoka 'kifungoni'

**Yapewa** leseni papo hapo, wadau wafunguka, sheria vyombo vya habari kufumuliwa...*Uk. 2 & 4*



NAPE NNAUYE

## Wabunge wavutana kuhusu sakata la Ngorongoro

UK. 5



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na viongozi mbalimbali baada ya kuwasili jijini Paris, Ufaransa jana, kushiriki mkutano wa wakuu wa nchi na serikali utakaojadili rasilimali bahari duniani. **PICHA: IKULU**

## Shahidi aliyeugua kizimbani akwamisha kesi Mbowe

UK. 2

MICHEZO SIMBA: TUTAWAPA RAHA WATANZANIA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6




Msemaji wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Payo Nzalayaimisi, (wa nne kulia), akipata maelezo kutoka kwa Kaimu Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Epson Luhwago (shati la bluu), alipotembelea ofisi hiyo pamoja na ujumbe wake katika chumba cha habari cha kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana, wakiwa kwenye ziara ya mafunzo katika vyombo vya habari vya IPP. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Magazeti maarufu yatoka 'kifungoni'

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ametangaza kuyafungulia magazeti manne yaliyokuwa yamefungiwa kwa zaidi ya miaka miwili kwa madai ya kukiuka miiko na maadili ya uandishi wa habari.

Magazeti hayo ni Mwanahalisi, Mawio, TanzaniaDaima na Mseto.

Nape alitangaza uamuzi huo wa serikali jana wakati akifungua mkutano wake na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini, kwa lengo la kujadiliana masuala yanayohusu tasnia hiyo.

Alisema ameyafungulia magazeti hayo na kukabidhi leseni ikiwa ni uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan. "Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Deudatus Balile, amezungumza hapa kuwa lilitolewa agizo la Rais la kufungulia vyombo vya habari. Agizo la Rais ni sheria na sheria inatekelezwa. Leo (jana) hapa tutatoa leseni kwa magazeti manne yaliyokuwa yamefungiwa," alisema Nape huku akipigiwa kofi.

Waziri Nape alisema kwa sababu serikali imeamua kutoka kwenye maneno lazima itende.

"Kama nimekuja nasema nia yetu ni njema, tuanze kwa kufungua ukurasa mpya si ndio eeh! Na leseni hizo nitazikabidhi mimi mwenyewe hapa ili tumalize kabisa. Sasa kama kuna mwenye maneno yake aseme mwenyewe. Kifungo kimetosha, kikubwa kazi iendelee," alisema Nape.

Aidha, alisema kwa pamoja wanajenga nchi moja, hivyo alivitaka vyombo vya habari kutumia nia njema ya serikali kwa sababu si kazi rahisi kufika hapa ilipofikia. "Nawaomba tunajenga nchi moja, sio kazi rahisi kufika hapa tulipofika, nataka kuwaomba tutumie vyema imani ya serikali. Kama lipo jambo tuongeeni," alisisitiza Nape. Awali, Balile akiwasilisha salamu za wahariri, alimwomba Nape kushughulikia mambo mawili ambayo ni Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ambazo ni kandamizi na kuvifungulia vyombo vya habari vilivyofungiwa.

"Kwanza nikupongeze kwa mara ya kwanza tukiwa mubashara, kwa uteuzi huu na viongozi wengine kwa uteuzi mlioupata. Naomba utaratibu huu wa leo wa kukutana uendelee ili kukuza mshikamano huu kati ya serikali na vyombo vya habari," alisema Balile. "Jambo linalovibana vyombo vya habari ni sheria zinawabana waandishi wa habari na Aprili 21, 2021, Rais Samia aliagiza vyombo vya habari vilivyofungiwa vifunguliwe. Tunaomba vifunguliwe kwa sababu vinachafua sura ya taifa letu kimataifa," aliongeza. Naye mmiliki wa magazeti ya Mawio na Mwanahalisi, Saed Kubenea, aliishukuru serikali ya Rais Samia na Waziri Nape kwa kufungulia vyombo hivyo vya habari. Alisema magazeti hayo yalishamaliza adhabu ya miaka miwili lakini hayakuwa yamerudi mitaani.

"Ni vizuri kusikilizana naahidi kufanya kazi kwa weledi, usalama wa nchi na kwa maslahi mapana ya nchi. Tulipopita tumepita, Mungu akubariki sana. "Tumepata leseni lakini unaweza usitukute mtaani, serikali iangalie namna ya kutoa ruzuku kwa vyombo vya habari binafsi," alisema Kubenea.

**WADAU WANENA**

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, alisema anafurahi kuona vyombo hivyo vimefunguliwa kwa kuwa tangu mwanzo walikuwa na hamu ya kuona vinaendelea kufanya kazi na ndio maana waliviunga mkono katika jitihada zao za kutafuta haki mahakamani.

"Baadhi ya hivi vyombo baada ya kufungiwa tuliviunga mkono kwenda mahakamani na baadhi kama Mwanahalisi viliamriwa kwamba virudishwe, kwa hiyo ni furaha yetu kuwa hatimaye serikali imesikiliza kilio cha wadau na uamuzi wa mahakama," alisema Kajubi.

Alisema licha ya serikali kufungulia vyombo hivyo, kuna umuhimu wa kubadilisha sheria kwa kurekebisha baadhi ya vipengele ili kuepusha kutumika kufungia vyombo vingine.

"Tunashukuru serikali imetamka nia ya kurekebisha hii sheria, tunasisitiza mchakato uanze na kama alivyoahidi waziri, tushirikishwe wadau wote katika mabadiliko hayo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA-TAN), Salome Kitomari, alisema kufunguliwa kwa vyombo ni tumaini jipya kwa tasnia ya habari ambayo ilidumaa kutokana na changamoto mbalimbali, sasa ni wakati wa wanatasnia kutumia nafasi hiyo vizuri kwa manufaa endelevu. "Hatuwezi kukwepa kujiendeleza ndilo takwa la dunia kwa sasa, tusiipe kisogo elimu bali tuyatafute maarifa kokote na kwa bidii kubwa," alisema Salome.

Kuhusu vyombo vya habari kupewa ruzuku, alisema ni jambo jema na serikali ya Tanzania haitakuwa ya kwanza kufanya hivyo kwa kuwa nchi kama Denmark inatoa zuruku kwa vyombo vyote kwa kuwa inaamini katika uhuru wa kujieleza na upatikanaji wa taarifa, kwamba hakuna mahali itawafanya waandishi au vyombo vya habari visitekeleze majukumu yake ya kuelimisha, kuburudisha na kukosoa.

**Ilmeandikwa na Jenifer Gilla, Mary Geoffrey**


**THE COMPANIES ACT, 2002**
**HOTEL CONTINENTAL LIMITED**
(REG. 6032)

**NOTICE OF RESOLUTION TO WIND UP VOLUNTARILY**

**NOTICE** is hereby given to the general public that by a special resolution dated 17th November 2021, the members of **HOTEL CONTINENTAL LIMITED** resolved to wind up the company voluntarily.

**FURTHER NOTICE** is given that, **I Ayoub Mtafya** was appointed Liquidator for purpose of winding up the company.

**TAKE FURTHER NOTICE** that all creditors of the company are hereby requested to furnish the Liquidator with full details of their claims against the company at the address shown below within fourteen (14) days from the date of this Notice. The claim (if any) shall be presented in the form known as "proof of a debt" (form 365) which is obtained at the offices of the Registrar of the Companies (BRELA) or can be downloaded from the website of BRELA.

Signed at Dar es Salaam this 8th day of February 2022.

**Ayoub Mtafya,**
**Liquidator,**
**Nexlaw Advocates,**
**4th Floor, PPF Tower,**
**P.O. Box 75578,**
**DAR ES SALAAM.**

216701302


# Shahidi aliyeugua kizimbani akwamisha kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa 13 wa Jamhuri katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, na wenzake watatu, Inspekta Tumaini Swila, aliyeugua ghafla juzi kizimbani, amekwama kufika mahakamani kwa madai ameshauriwa na daktari apumzike.

Kesi hiyo ilitakiwa kuendelea kusikilizwa jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joachim Tiganga lakini iliahirishwa.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, akiiwakilisha Jamhuri, alidai kuwa shahidi hakufika mahakamani kuendelea na ushahidi na ameshauriwa na daktari apumzike, hivyo hawawezi kuendelea kinyume cha ushauri wa daktari. "Tungeweza kutafuta shahidi mwingine wa kuendelea naye isipokuwa kwa muda wa jana (juzi) na leo (jana) isingetosha kutafuta shahidi mwingine.

"Naomba kuahirishwa kesi hadi Jumatatu kama shahidi atakuwa hajapona tunaweza kutafuta shahidi mwingine. Shahidi katuma nakala za cheti, nakala halisi atakuja nayo atakapopona," alidai wakili Tatuga.

Akijibu Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, alidai walitaka alete nyaraka kutoka hospitali ya serikali na wanasisitiza kwamba kwa mujibu wa sheria shauri hilo linatakiwa liwe limemalizika ndani ya miezi tisa.

"Tukienda kwa mwenendo huu tutakuja kuomba muda wa nyongeza. Jumatatu mbali tuendelee kesho (leo). Jamhuri wana akiba ya mashahidi 11, wawalete tuendeleee," alidai Kibatala.

Wakili Katuga alirejea kujibu hoja za Wakili Kibatala akidai hakubaliani na hoja ya kuendelea na shauri siku ya Jumatatu kwa kuwa wanaweza kufika na hadithi ya kukosa shahidi.

Aliomba shauri liendelee Jumatatu kama shahidi atakuwa hajapona na shahidi mwingine anatakiwa asafiri atakuwa amefika.

Baada ya kusikiliza hoja hizo, Jaji Tiganga alisema mahakama ina nia ya kumaliza shauri hilo kwa haraka.

Alisema kwa sababu zilizotolewa, mahakama inaahirisha shauri hilo hadi siku ya Jumatatu wiki ijayo saa tatu asubuhi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Halfani ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama, kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020.

# HABARI KITAIFA




Mtaalamu wa Sheria kutoka Mpango wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA), Harvey Kombe (kushoto), akitoa elimu kwa wafanyabiashara wa Soko la Nguzonane, Manispaa ya Shinyanga juzi, kuhusu kufanya biashara kwa mfumo rasmi na kuchangamkia fursa za mikopo kwenye taasisi za kifedha ili wapanue wigo wa kibiashara na kukua kiuchumi. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Wanafamilia wauawa madai wizi pikipiki

**Na Waandishi Wetu, MOSHI**

WATU watatu wa familia moja, wameuawa na wawili kati yao miili yao imeteketezwa kwa moto katika Kijiji cha Manushi Ndoo, Kata ya Kibosho Magharibi, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Akizungumzia tukio hilo jana, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Manushi Ndoo, Alex Kway maarufu Kenche, alisema ndugu hao walipoteza maisha, baada ya kuvamiwa na kundi la vijana, waliowashambulia wakiwatuhumu kuiba pikipiki eneo la Kijiweni, Lyamungo, Tarafa ya Machame, Wilaya ya Hai.

"Ni kweli hao waliouawa ni wananchi wangu. Wawili kati yao walipigwa mawe na kuchomwa moto hadi kufariki dunia, na ndugu mwingine wa tatu, naye alikatwa panga shingoni na kufariki papo hapo.

"Hilo tukio lilitokea usiku wa kuamkia jana, majira ya saa 1:00 usiku wa Februari 9, mwaka huu. Walipigwa kuanzia saa 11:00 jioni na baadaye kuchomwa moto saa 1:00 jioni," alisema.

Aliwataja waliouawa kuwa ni Marious Mmasi, Ombeni Mmasi, ambao wanadhaniwa kuwa na umri kati ya miaka 45 hadi 50. Na mwingine ni mdogo wao aitwaye Anold Mmasi au jina jingine Sikujua.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kijiji hicho, ndugu hao waliouawa walikutwa wakiwa wanaendesha pikipiki hiyo ya wizi.

"Inadaiwa kwamba hawa ndugu wa familia moja, walikuwa wanaitumia hiyo pikipiki kwa siku nne au tano hivi. Hao vijana walioibiwa huko Lyamungo wakafanya uchunguzi wao na wakajua kuwa mali yao iko Manushi Ndoo.

"Walipogundua wakaanza safari kuja huku kijijini eneo linaloitwa kwa Rafaeli karibu na kanisa la TAG (Tanzania Assemblies of God). Wakawa wameweka mtego wao na kujiandaa kwa usafiri wa pikipiki na gari," alisema.

Aidha, inadaiwa kuwa vijana waliotekeleza mauaji hayo, walikuwa wa kati ya 30 na 40. Wakati mauaji hayo yanafanyika, marehemu Marious alikuwa amembeba mdogo wake Ombeni katika pikipiki hiyo, lakini Anold aliuawa baadaye kwa panga alipodai godoro la kaka yake. Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, Diwani wa Kibosho Magharibi, Prosper Mallya, alisema alipata taarifa za mauaji ya ndugu hao wa familia moja, majira ya saa 3:00 usiku.

"Nikiwa natokea kwenye mihangaiko yangu, nilipata taarifa za ndugu wawili kuuawa kwa kuchomwa moto, wakituhumiwa kukutwa na pikipiki ya wizi kutoka Machame. Sasa wakati nafuatilia undani wa tukio hilo, ili nitoe taarifa Polisi, nikapewa taarifa ya tukio jingine la ndugu wa familia hiyo kuuawa kwa kukatwa panga," alisema.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Maria Daniel, alisema wakati wa uhai wao, vijana hao wote watatu walikuwa wakituhumiwa kuhusika katika moja ya kesi ya mauaji, ambapo miaka miwili iliyopita, walishinda kesi hiyo mahakamani.

"Hatufurahii kifo cha hawa vijana, tunatambua wana watoto na wazazi, lakini walishakuwa tishio kwa kata hii," alisema mkazi huyo.

●**Imeandikwa na Anjela Mhando na Mary Mosha**

## Majaliwa aagiza hatua upandishaji bei bidhaa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameeleza sababu za kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali nchini kuwa ni pamoja na wafanyabiashara kuzalisha kwa kiwango kidogo ili kutengeneza uhitaji.

Kutokana na hali hiyo, ameagiza Tume ya Ushindani (FCC) kukagua uzalishaji viwandani na kuwaonya wafanyabiashara wanaotengeneza upungufu ili kuumiza wananchi kwa kupandisha bei.

Majaliwa alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Msalala (CCM), Idd Kassim, ambaye alisema kumekuwapo na ongezeko la bei za bidhaa mbalimbali nchini hasa Shinyanga jimbo la Msalala hususan mafuta ya kula, vifaa vya ujenzi kama nondo na saruji. Alihoji nini kauli ya serikali juu ya ongezeko au mfumuko wa bei kwa bidhaa.

Akijibu swali hilo, Majaliwa alikiri kumejitokeza siku za hivi karibuni kupanda kwa bei za baadhi ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. "Upandaji wa bei hizi wakati mwingine ni kakusudi unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara ambao si waaminifu lakini pia upatikanaji wa malighafi, viwanda vyote vinavyozalisha hapa nchini vingi vinategemea malighafi hapa nchini na malighafi zipo,"alisema.

Alisema upo mkakati wa wafanyabiashara waovu wasio na nia nje wanapandisha bidhaa kwa makusudi na wanazalisha kidogo sana ili kutengeneza upungufu mtaani na bei zipande.

"Pia kumekuwa na utamaduni wa wafanyabishara waovu kakaa pamoja kujadili bei ziweje na kusababisha mfumuko wa bei, sisi serikali tumelibaini hilo, Waziri Kijaji (Ashattu) ametoka hadharani kueleza mkakati wa serikali naunga mkono kauli yake,"alisema.

Aliagiza wafanyabiashara kuacha tabia hiyo ovu inayosababisha jamii kushindwa kupata bidhaa kwa gharama nafuu.

"Kwasababu wakati tunawekeana mikataba na kujenga mazingira rahisi ya uwekezaji nchini lengo la kwanza lilikuwa ni kupata bidhaa kwa wingi, kwa bei nafuu na zipatikane wakati wote sasa wengine wameanza kukiuka masharti yetu."

## CCM yaahidi kusaidia matibabu ya Prof. Jay

**Na Beatrice Shayo**

VIONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamemtembelea na kuahidi kuendelea kumsaidia katika matibabu yake, aliyekuwa Mbunge wa Mikumi (CHADEMA), Joseph Haule, maarufu Profesa Jay, aliyelazwa kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo na Katibu wa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, jana walikwenda hospitalini huko kumjulia hali.

Profesa Jay ambaye pia ni msanii wa muziki wa kizazi kipya, aliripotiwa kulazwa hospitalini huko tangu mwezi uliopita akiwa chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu (ICU).

Katika taarifa yake jana, Chongolo alisema: "Tumemwona ndugu yetu Profesa Jay, hali yake inazidi kuimarika, tumshukuru Mungu lakini niwashukuru madaktari kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kumhudumia, pamoja na mchango huu wa kuwezesha matatibu.

"Kwa niaba ya Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, niwahakikishie tutaendelea kutoa kila aina ya ushirikiano katika kuhakikisha matibabu yanaendelea vyema huku tukiendelea kumwombea apone haraka."

Juzi katika mitandao ya kijamii kulisambazwa tangazo la kuomba michango kwa ajili ya matibabu ya msanii huyo, likiwa na kibali cha mkewe anayeitwa Grace Mgonja.

Grace alifafanua kuwa walemazimika kuomba msaada huo kwa kuwa kwa wiki moja wanatumia hadi Sh. milioni nne kwa ajili ya matibabu ya mumewe.

"Mwisho wa siku huyu ni mtu wa watu, kila wakati simu na ujumbe haukatiki, wengine wanataka kusaidia, tukaona turuhusu wamsaidie," alisema Grace.

Alisema wakati wanaanza matibabu, waliwasiliana na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ambaye aliwasiliana na familia kupitia Naibu Waziri wake, Dk. Godwin Mollel na wanashukuru kwa huduma walizopatiwa hospitalini huko.

Alisema wapo baadhi ya wabunge na viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na CCM wanawapatia ushirikiano na kutaka kujua hali yake.

Alitangaza namba za kuchangia matibabu ya Professa Jay kuwa ni 0757 919 192 au 0715 919192 zenye jina la Joseph Haule na kwa benki ya CRDB namba 0112044845200 yenye jina la Joseph Haule.

Profesa Jay katika sanaa yake amewahi kutesa na vibao mbalimbali ikiwamo 'Ndio Mzee', 'Zali la Mentali', 'Jina Langu', 'Nikusaidiaje', 'Kama Ipo' na 'Kipi Sijasikia'.

JAMBO AFRICA'S WEB3 SUPERAPP




Ni mchezo wa kujifunza fursa na pia katika mchezo huu unaweza kulipwa.
Kwa maelezo zaidi tembeleaTwitter@jambotechnology,
YouTube@jambo technology au tovuti yetu.
WWW.JAMBO.TECHNOLOGY/SIGNUP
116699602

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
10 – 02 - 2022

TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumanne tarehe 15-02-2022 hadi 28-02-2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea JNHPP SITE,** gari hilo lenye namba za usajili:
   **T 203 DJY / T 837 DJB**
   **T 204 DJY / T 887 DJB**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 20.60**
   **Upana - mita 4.83**
   **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM hadi JNHPP SITE kupitia MKURANGA, KIBITI, MLOKA.** Gari litasafiri muda wa mchana tu *(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)*

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*
216701202

# Sheria vyombo vya habari kufumuliwa

Na Mary Geofrey

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameagiza kupitiwa upya kwa sheria, sera, kanuni na taratibu za vyombo vya habari nchini, kwa lengo la kurahisisha utendaji kazi na kuongeza mshikamano na serikali.

Aidha, serikali imeongeza muda wa mwaka mmoja kwa wanahabari kujiendeleza na kufikia ngazi ya stashahada.

Rais Samia alitoa maagizo hayo kupitia kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, aliyewasilisha kwa niaba yake jana mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye kikao kazi chake na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari jana, Nape alisema hayo ni maagizo ya Rais Samia kuboresha sheria hiyo baada ya kupokea maoni ya wadua wa sekta hiyo.

"Serikali tunataka kuboresha uhusiano uliopo na mimi najua tulipotoka, tuboreshe uhusiano kati ya wanahabari, sekta ya habari na serikali. Tuboreshe kadri inavyowezekana. Rais ameelekeza tupitie sheria, sera, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya habari na kuona namna ya kuzifanya ziwe rafiki na kuwezesha utendaji kazi wa wanahabari badala ya kuwa kikwazo kwa wanahabari," alisema.

Nape aliiagiza Idara ya Habari (MAELEZO) ndani ya muda mfupi iandae kikao cha wadau wa habari kujadili mapendekezo ya marekebisho ya habari kwa lengo la kutengeneza kamati ndogo itakayopitia kifungu kwa kifungu ili kupata maboresho mapya ya sheria ya habari.

**MADAI YALIPWE**

Nape alisisitiza kuwa wakati wakipitia hayo mambo mengine lazima yaendelee mfano suala la madai ya waandishi wa habari na kwamba vyombo vya habari vinavyodaiwa na waandishi wa habari viwalipe.

"Wamiliki waendelee kulipa haki za waandishi wa habari kuwalipa ni haki yao. Yenye utata tutaendelea kutumia katiba, taratibu, kanuni na busara, mengine tutaendelea kutumia busara," alisema Nape.

"Nimekuja kuzungumza na nyie kueleza muelekeo wa serikali inayoongozwa na Rais Samia, kwenye tasnia yetu ya habari, hili tunalolifanya hapa leo ni moja ya maagizo ya Rais Samia kwamba tuwe karibu na tasnia ya habari. Tubadilishane mawazo na tutumie tulichonacho serikalini kuongeza uwezo, tukae tuzungumze tuone namna ambavyo tutaenda pamoja kwa sababu ninyi ni wadau kwenye safari ya maendeleo ya nchi," alisema Nape.

Aliendelea kusema kuwa safari ya mabadiliko inachukua muda lakini kazi lazima ziendelee. "Ninachotaka tuaminiane, nimekuja kuwaomba wanahabari mimi mwenzenu naomba tuaminiane mimi 'degree' yangu ya kwanza ni ya habari kwa hiyo mimi ni mwandishi wa habari."

**KAULI YENYE UTATA**

Nape alitoa kauli ya safari ndefu ya kukutana na jiwe hupaswi kupasua jiwe, unatakiwa kurudi nyuma kutafuta njia ya kukwepa jiwe ili kuendelea na safari.

"Unaporudi nyuma haimaanishi umeamua kuahirisha safari bali unakuwa unatafuta njia rahisi ya kuendelea na safari," alisema Nape huku wanahabari wakifurahia kauli hiyo.

**MATANGAZO RUKSA**

Kadhalika Nape alizielekeza taasisi ambazo zilikuwa zinasita kutoa matangazo kwa vyombo vya habari pamoja na kulipa madai waendelee kufanya hivyo.

"Hakuna haja ya kubaguana wote wana haki sawa. Wote wapewe fursa, waweke utaratibu wa usawa. Ikiwezekana matangazo ya serikali yatoke kwa awamu katika vyombo tofauti tofauti awamu hii mkimpa huyu awamu ijayo mwingine, tusipotoa matangazo vyombo vya habari vitajiendeshaje?" alihoji Nape.

Aliwataka watendaji wa wizara yake kuwa wepesi wa kutoa taarifa zenye weledi ili kuepuka waandishi wa habari kuandika habari ambazo hazina sauti ya serikali.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Jimmy Yonazi, aliwapongeza wahariri wa vyombo vya habari kwa kazi kubwa wanayofanya ikiwa ni sehemu ya vyombo vya ulinzi na usalama wa nchi.

Aliwataka wahariri wa vyombo vya habari kufanya kazi na serikali ili sekta hiyo ikue ili wawekezaji waje kuwekeza nchini na sekta nyingine kwenda kuwekeza nchi nyingine.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Uongozi Instute, Balozi Ombeni Sefue, alisema wana jukumu la kutoa elimu kwa waandishi wa habari na namna ya kujenga uhusiano mzuri kati ya serikali na wanahabari ili kujenga serikali bora.

## Waumini KKKT wapigwa radi

Na Gurian Adolf, NKASI

WAUMINI 16 wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Kijiji cha Katani Kata ya Nkandasi wilayani Nkasi mkoani Rukwa, wamenusurika kifo baada ya kupigwa radi wakati wakifanya kazi za kilimo kwenye shamba la kanisa hilo.

Tukio hilo lilitokea jana kijijini hapo ambapo waumini wanane walijeruhiwa na kukimbizwa katika zahanati ya Kijiji cha Chala na kupatiwa matibabu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Katani, Jofrey Kisato, alisema tukio hilo lilitokea saa nane mchana shambani wakiwa kwenye mapumziko kwa ajili ya chakula.

Alisema wakati wakiendelea kula kukiwa na dalili ya mvua kunyesha ndipo ghafla ilipiga radi na kuleta taharuki kubwa.

Alisema baada ya radi kupiga waumini wote 16 walizimia na baadae walizinduka huku wanane kati yao hali zao zikiwa mbaya.

Alisema wanane walikimbizwa katika zahanati na baada ya kupata nafuu wote 16 walipelekwa Hospitali ya Kristo Mfalme Sumbawanga mjini kwa uchunguzi zaidi.

Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, William Mwampaghale, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuongeza kuwa ni vizuri wananchi wakachukua tahadhari katika kipindi hiki ambapo mvua kubwa zinanyesha zikiambatana na radi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Prof. Lawrence Museru (wa pili kushoto), akionyesha cheti cha Ithibati ya Ubora, kutoka Shirika la Viwango vya Ukaguzi Kimataifa kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADCAS), alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Naibu Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Julieth Magandi, Ofisa Ubora-Maabara, Dk. Lanja Kahemela (kulia) na Mkurugenzi Tiba na Huduma Shirikishi, Dk. Luku Sakafu. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Hospitali ya Mloganzila yapata ithibati kimataifa

Na Christina Mwakangale

MAABARA ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili-Mloganzila, imeingia kwenye orodha ya maabara zinazotoa huduma bora duniani baada ya kutunukiwa cheti cha Ithibati ya Ubora kutoka Shirika la Viwango vya Ukaguzi Kimataifa kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na Kusini mwa Afrika (SADCAS),

Kadhalika, maabara hiyo ina uwezo wa kupima vipimo 1,000 kwa siku, ingawa hivi sasa vinavyofika kupimwa hospitalini hapo ni 400 pekee.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Prof. Lawrence Museru, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari na kuitaja ithibati hiyo yenye namba ISO 15189:2012.

"Haya ni mafanikio makubwa sana kwa maabara yetu kutambulika kimataifa. Ithibati hii imetokana na SADCAS kujiridhisha na ubora wa vipimo na majibu yanayotolewa na maabara ya Hospitali ya Mloganzila, kuthibitisha vitu mbalimbali, ikiwamo miongozo, uwezo wa wataalamu, ufanisi wa vifaa tiba na miundombinu ya aina 17 za vipimo.

"Vipimo vilihakikiwa ili kujiridhisha na kubainika vimekidhi viwango vya kimataifa kama inavyoelekezwa. Umuhimu wa ithibati hii itakuwa na faida mbalimbali kwa hospitali na kwa taifa," alisema Prof. Museru.

Alisema ubora huo wa maabara una manufaa kwa taifa na kwamba mbali na kutoa huduma inakuza biashara kutokana na maabara hiyo kupima kwa kutumia teknolojia ya kisasa inayotumia muda mfupi usiozidi nusu saa hadi saa moja.

"Vipimo 17 ambavyo hupimwa na maabara hii ni vile hata ambavyo ni muhimu kwa wanaohitaji kusafiri au kupata VISA na tunapima kutambua mikrobaolojia, bakteria, virusi. Sasa vipimo vitaaminika duniani," alisema Prof. Museru.

Alibainisha kwamba vipimo na majibu ya maabara hiyo yatatambulika kimataifa, kuaminika kwa ubora wa vipimo na majibu hivyo sampuli ya vimelea vitakavyopimwa katika maabara, vinaweza kutumiwa na mamlaka au taasisi yoyote duniani.

"Maabara hii itakuwa ni kituo cha mafunzo na utafiti wa vimelea mbalimbali kutokana na ubora huduma zake, kupokea na kupima sampuli kutoka nchi yoyote duniani na kutoa majibu sahihi na kwa wakati," alisema.

Kadhalika, alibainisha kwamba, maabara hiyo itakuza mahusiano mazuri kati ya maabara na hospitali hiyo na mabaara zingine ndani na nje ya nchi na pia Wizara ya Afya, iliweka mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma za maabara nchini kufikia kiwango cha kimataifa.

"Maboresho ya kuboresha maabara takribani 25 zinazotoa huduma za kimatibabu ya afya nchini Tanzania. Maabara ya MNH-Mloganzila ni miongoni mwa maabara 25 zilizokuwa zikitekeleza sera hiyo, imefanikiwa kufanya vizuri na kushika nafasi ya kwanza," alisema Prof. Museru.

## Miradi ya NHC iliyokwama kuendelezwa

**Na Munir Shemweta**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amesema serikali imedhamiria kuendelea na ujenzi wa miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) iliyosimama.

Miradi ya NHC iliyokwama Dar es Salaam pamoja Kawe na Morocco Square, ilisimama tangu mwaka 2017 kutokana na changamoto mbalimbali zikiwamo za kifedha na mabadiliko ya baadhi ya maboresho kwenye majengo ya Morocco Square.

Ridhiwani alisema hayo jana Bungeni wakati akichangia hoja iliyowasilishwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

"Serikali iko tayari kukamilisha miradi iliyokuwa imesimama na inayojengwa katika Kiwanja No. 300 Regent Estate, Kiwanja No. 711 na Moroco Square," alisema Ridhiwani.

Alisema serikali imefanya juhudi kubwa kuhakikisha miradi ya NHC iliyokwama inakamilika ili ikae vizuri na katika hatua ilizofanya NHC ni kuomba kuchukua fedha kutoka vyanzo vyake vingine au kukopa katika taasisi za fedha ili kukamilisha miradi iliyokwama.

Hata hivyo, Ridhiwani aliwaambia wabunge kuwa serikali ilielekeza kamati inayosimamia madeni iangalie vizuri yale yaliyoombwa na NHC. Alisema katika kuchakata kwake, liliruhusiwa shirika kukopa Sh. bilioni 44.7 ili kukamilisha miradi hiyo.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Ardhi, kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 19 zinaenda Kitalu Na. 300 na kiasi kilichobaki kiende kwenye mradi wa Morocco Square.

Kuhusu eneo la Kawe, alisema maelekezo ni kuwa shirika likae na mwekezaji mwenza, kampuni ya Al-Gurey Dubai kuona namna bora ya kuendelea na mradi huo.

Naibu Waziri alisema, baada ya mazungumzo na mwekezaji mwenza, hatua iliyofikiwa baada ya mikutano mitatu ni kwamba anaenda kuwasiliana na wenzake ili mambo watakayokubaliwa waje kuzungumza kwa pamoja.

# Wabunge wavutana kuhusu Ngorongoro

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WABUNGE wamevutana kuhusu kuondolewa, kupunguzwa kwa watu na mifugo ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) huku baadhi wakidai mifugo inamilikiwa na matajiri wachache na wananchi wakiwa maskini.

Wakijadili bungeni jana, baadhi ya wabunge walisema wananchi hao hawako ndani ya eneo hilo kwa bahati mbaya bali kisheria na kwamba wanastahili haki zote za msingi.

Kutokana na mvutano huo, serikali ilitoa msimamo kuwa itawasilisha muswada wa mabadiliko ya sheria ya uanzishwaji wa NCAA, huku Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiahidi kuwa timu ya serikali itakwenda kuzungumza na wananchi na wale wa Loliondo ili kupata suluhu huku akisisitiza haki za binadamu zitalindwa.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alisema ni muhimu Bunge likatafakari mgogoro uliopo tarafa ya Ngorongoro yenye kilomita za mraba 8,000 ambalo kuna maisha mseto yaliyoanza tangu mwaka 1959.

Alisema mgogoro mwingine ni tarafa ya Loliondo yenye ukubwa wa kilomita za mraba 5,000 za pori tengefu na kwamba wakati serikali inafanya tathmini, ni muhimu bunge likaelewa upotoshaji unaoendelea ni mkubwa na hauwatendei haki wananchi hao.

"Wamasai wamekuwa waungwana kwenye uhifadhi. Kama kuna kabila lilionyesha uhifadhi bora na kuishi na wanyama katika eneo moja bila kuwadhuru ni tarafa ya Ngorongoro na kwamba walitoa ardhi ya Serengeti, Tarangire, Lake Manyara na leo kilomita za mraba 1,500 ambazo zilishaundiwa tume na kuleta taarifa na Waziri Mkuu, Mizengo Pinda wakati huo alitoa uamuzi," alisema.

Sendeka pia alisema Rais (wa awamu ya nne) Jakaya Kikwete alisema hakuna mpango wa serikali kuwanyang'anya Wamasai eneo lao na kwamba kwa sasa usimamizi hafifu umechangia mgogoro huo kukua.

Mbunge wa Ngorongoro, Emmanuel Lekishoni, alisema eneo la Ngorongoro haliwezi kufa kwa sababu wananchi walioko ni wahifadhi tofauti na wahifadhi wa vitabuni na kwamba wameishi miaka 60 bila kuua wanyama na kuwadhuru.

"Leo hii wananchi hawa wanaonekana ni watu maskini, wavamizi na wasiofaa, watoto wanaenda shule, kuna vituo vya afya, zahanati. Kama tumefika mahali tunaona ni tatizo lazima kukaa na wananchi kutafuta suluhu. Nashauri kamati na wizara ni lazima kukaa na wananchi ila kwa sasa kuna uadui mkubwa kati ya wizara na wananchi. Tunajua hawajavamia waliingia mkataba na mkoloni kuhama Serengeti kuja Ngorongoro," alisema.

Kwa mujibu wa Mbunge huyo, Pori Tengefu la Loliondo lilitangazwa pamoja na mengine 40 mwaka 1974 na waziri alitakiwa kutangaza ndani ya miezi 12 na haikufanyika hivyo huku idadi ya watu ikiongozeka na sasa ni zaidi ya 80,000 vijiji 23 na kata nane na zikitolewa kilomita 1,500 wananchi hawatakuwa na sehemu ya malisho wala pa kuishi.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonda, alisema ushirikishwaji ni muhimu pamoja na kuzingatia haki za binadamu ili kulinda hifadhi na uendelevu wake.

Naye Hassan Mtenga (Mtwara Vijijini) alisema haiwezekani kuwa na hifadhi yenye zaidi ya watu 100,000 na zaidi ya mifugo 800,000 na kwamba eneo hilo hilo linaongoza kwa kukusanya mapato na kwamba mwaka 2018 walikusanya Sh. bilioni 148 ambazo yanasaidia wananchi wote.

Mtenga alisema Mtwara kulikuwa na mradi wa gesi uliozua mambo mengi na serikali ilichukua maamuzi na gesi ilitoka kwa Watanzania wote, lakini kwa suala la NCAA maslahi ya taifa hayaangaliwi.



Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka



Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba

Aidha, alisema Baraza la Wafugaji ndiyo chanzo cha mgogoro na kwamba wanapewa Sh. bilioni tatu kwa mwaka kuendesha shughuli zao ambazo zinageuka kuwa chungu kwa serikali. "Kama mlipeleka vifaru Mtwara na vitu vingine ili gesi iwe keki ya taifa basi ya NCAA hatua zichukuliwe. Kama mling'ata jongoo Mtwara basi Ngorongoro hatua zichukuliwe au kwa sababu kuna matajiri," alisema.

Naye Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba alisema hadhi iliyo nayo Ngorongoro ni kubwa duniani kwa kuwa ina utalii wa miamba na kwamba kupanga ni kuchagua liwe eneo la wanyama au binadamu.

"Nimefika NCAA hali ni mbaya. Kuna zaidi ya mifugo 800,000 inayomilikiwa na wazawa lakini asilimia tatu swali ile mingine inamilikiwa na nani? Ukitaka kujua hilo leo Waziri Mkuu tangaza kwamba wale wananchi ng'ombe wanaomiliki wote wawe wao utaona anapigwa mwingine analia mwingine," alisema.

Mbunge Salome alisema wananchi hao wanafuga kondoo ambao hung'oa majani na mizizi na matokeo yake itaota mimea ambayo siyo rafiki kwa uhifadhi, na kwamba kuna wanaotetea maslahi yao na siyo ya taifa.

Alisema mwaka jana zaidi ya tembo 20 na faru mmoja waliuawa ambao waliwekewa sumu na kwamba nchi inahitaji iambiwe na nani kwamba NCAA ni urithi wa taifa na mali ya Watanzania.

Naye Mbunge wa Mvumi, Livingstone Lusinde, alisema ni muhimu serikali ikaleta Muswada wa Mabadiliko ya Sheria na kulinda haki za kila mmoja na kwamba ni lazima wananchi waondolewe eneo hilo kulinda hifadhi hiyo.

Akijumuisha hoja hizo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, alisema serikali italinda na kuheshimu haki za binadamu na inatagemea kuwasilisha muswada wa mabadiliko ya sheria iliyoanzisha NCAA.




Hallmark Attorneys

EXIM BANK
Innovation is life

**NOTICE TO THE OCCUPIERS**
**OF FIFTY (50) UNITS IN UHURU HEIGHTS TOWER– DAR ES SALAAM UNDER RECEIVERSHIP**

I, Walter Buxton Chipeta, the Receiver/Manager of Hallmark Attorneys of P.O. Box 13811, Dar es Salaam, hereby give notice to the occupiers of the following 50 Units, all comprised on Plot No. 63/17 Upanga, Dar es Salaam, under receivership, as follows:

| S/N | CT NO. | APT NO. | S/N | CT NO. | APT NO. | S/N | CT NO. | APT NO. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 38083/4 | D 10th Fl | 18 | 38083/134 | B 18th Fl | 35 | 38083/210 | P 6th Fl |
| 2 | 38083/10 | D 11th Fl | 19 | 38083/135 | E 16th Fl | 36 | 38083/211 | P 7th Fl |
| 3 | 38083/11 | E 11th Fl | 20 | 38083/136 | E 15th Fl | 37 | 38083/212 | P 7th Fl |
| 4 | 38083/17 | F 12th Fl | 21 | 38083/137 | D 15th Fl | 38 | 38083/213 | PH |
| 5 | 38083/18 | E 12th Fl | 22 | 38083/138 | B 15th Fl | 39 | 38083/214 | Ofc 9th Fl |
| 6 | 38083/23 | E 13th Fl | 23 | 38083/161 | E 21st Fl | 40 | 38083/215 | P1 1st Fl |
| 7 | 38083/31 | P1 1st Fl | 24 | 38083/162 | D 20th Fl | 41 | 38083/216 | P2 2nd Fl |
| 8 | 38083/32 | P2 2nd Fl | 25 | 38083/176 | D 16th Fl | 42 | 38083/217 | P3 3rd Fl |
| 9 | 38083/33 | P3 3rd Fl | 26 | 38083/180 | Shop N.4 | 43 | 38083/218 | P5 5th Fl |
| 10 | 38083/36 | P6 6th Fl | 27 | 38083/198 | ShopN.21 | 44 | 38083/219 | P6 6th Fl |
| 11 | 38083/38 | P8 9th Fl | 28 | 38083/201 | ShopN.25 | 45 | 38083/220 | P7 7th Fl |
| 12 | 38083/89 | A 20th Fl | 29 | 38083/204 | ShopN.26 | 46 | 38083/221 | P9 9th Fl |
| 13 | 38083/127 | B PH | 30 | 38083/205 | ShopN.29 | 47 | 38083/222 | P8 8th Fl |
| 14 | 38083/128 | F 23rd Fl | 31 | 38083/206 | P 2nd Fl | 48 | 38083/223 | C5 1st Fl |
| 15 | 38083/129 | F 23rd Fl | 32 | 38083/207 | P 3rd Fl | 49 | 38083/224 | ShopN30 |
| 16 | 38083/131 | F 24th Fl | 33 | 38083/208 | P 4th Fl | 50 | 38083/225 | Ofc. P-4 |
| 17 | 38083/133 | B 18th Fl | 34 | 38083/209 | P 6th Fl | | | |

**TAKE NOTE THAT** effective 17th January 2022 following my appointment as Receiver/Manager, you as the OCCUPIERS of the charged properties are legally bound to account to me on the status of your occupation thereof and by this notice are required to do so within five (5) days, by 16th February 2022, at 17.00 hours as follows:

1. Submit all relevant details of your occupation of the charged property in writing;
2. Submit your full names and contact information including mobile numbers and emails;
3. Submit copies of all leases, agreements and or subleases of the charged property; and
4. Submit proof of all payments made in relation to your occupation of the charged property from inception up to and including 31st January 2022

**TAKE NOTICE THAT** strict legal measures will be taken against you, jointly and or severally, for noted non-compliance with the terms of this notice and the law.

All correspondences, information and or clarifications to be issued through the Receiver/Manager's address hereinbelow.

**WALTER BUXTON CHIPETA**
**RECEIVER/MANAGER**
**C/O HALLMARK ATTORNEYS**
**18 RUVU/ CHOLE ROAD,**
**MASAKI AREA**
**P. O. BOX 13811,**
**DAR ES SALAAM.**
**Tel: +255 22 2601 314/6**
**Email: info@hallmarkattorneys.co.tz**

116699702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mfumo kutoa watoto mitaani uharakishwe

**KATIKA** miji mbalimbali nchini, kumekuwapo na wimbi la watoto wa mitaani ambao wamekuwa wakilandalanda kandokando ya barabara kuomba msaada wa fedha kwa madereva wa magari na hata abiria katika mabasi.

Baadhi ya watoto hao ambao wengi wao wana umri wa kuwa shule ya msingi, husafisha vioo vya magari ya kibafsi kisha kuomba wapewe fedha hata kama hawakuruhusiwa kufanya hivyo na wamiliki wa magari hayo.

Katika mazingira hayo, wakati mwingine hutaka walipwe kwa lazima, na wasipopewa, hudiriki hata kuwamwagia maji machafu madereva wanawake kama shinikizo la kutaka walipwe fedha.

Lakini imekuwa ikidaiwa kuwa wakati watoto wakiwa kando ya barabara wakiomba fedha, wazazi au walezi wao huwa wamejificha maeneo ya karibu wakisubiri kuletwa makusanyo ya fedha kutoka kwa watoto hao.

Ili kumaliza wimbi la watoto hao mitaani, kumekuwapo na jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali za kuwarudisha kwao, lakini bado hazijazaa matunda kutokana na kuendelea kuonekana mitaani.

Hata hivyo, sasa serikali imetangaza kuanzisha mfumo maalumu utakaowezesha kuwaondoa mitaani huku ikiagiza walioko nyumbani kwa wazazi wao au walezi kubakia huko.

Katika kufanikisha hilo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Doroth Gwajima, anasema serikali inaandaa mpango utakaokomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Kwanza tunaipongeza serikali kwa kutangaza mfumo wa kuondoa watoto hao mitaani, kutokana na ukweli kwamba, wanakwama kupata elimu ambayo ingewasaidia kutimiza ndoto zao za baadaye.

Mambo ya ukatili wa kijinsia, yanatajwa kuchangia kuwapo watoto wa mitaani, ambapo waziri anasema serikali ina mpango wa kukabiliana na tatizo hilo na kuwezesha familia za watoto wa mitaani ili zijimudu kwa kipato.

Tunaamini kwamba, kwa utaratibu huo, inawezekana watoto wakapungua mitaani na kubaki kwa wazazi au walezi na kupelekwa shule ili kupata elimu, kwani elimu ni miongoni mwa haki zao za msingi.

Lakini pamoja na hayo, tunadhani ipo haja ya kuweka mipango ya mikakati ambayo itahakikisha hakuna mtoto wa mtaani au ombaomba yeyote, kwani baadhi yao ndiyo huwatumia watoto kuomba, huku wao wakiwa wamejificha.

Tunashauri hivyo, kwa sababu uzoefu unaonyesha kuwa kila ombaomba na watoto wao wakiondolewa mitaani na kupelekwa kwao, baada ya miezi michache hurudi na kuendelea na kazi ya kuomba misaada.

Kwa mfano, jijini Dar es Salaam, mara kadhaa viongozi wa serikali wamewahi kufanya jitihada za kuwaondoa ombaomba wakiwamo watoto wanaozurura mitaani, lakini baada ya miezi michache huwa wamerejea.

Hivyo, tunashauri kuwa mfumo ambao umetangazwa na waziri kwa ajili ya kuondoa watoto mitaani, ulete matokeo chanya, kwani inawezekana katika kundi hilo wapo viongozi na wataalamu wa fani mbalimbali wa baadaye.

Kimsingi, tunaona kwamba, watoto hao kudhurura mitaani wanaweza kuiga tabia mbaya ambazo wakati mwingine zinaweza kuwafanya wawe watu hatari wa baadaye, hivyo wangewezeshwa kupata elimu.

Tunatarajia kwamba mfumo huo utarahisishwa kwa lengo la kuwanusuru watoto wetu ili wapate haki ya elimu na kuwa nguvukazi ya taifa ya baadaye badala ya kutumikishwa na kuwa wahalifu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



# Hongera Magu kwa kujipanga miradi miundombinu, ila udhibiti muhimu

Na Anthony Gervas, Mwanza.

**SERIKALI** ilivyoamua kumwaga mabilioni ya shilingi katika halmashauri mbalimbali za wilaya, miji na mikoa nchini ni jambo la faraja. Kwani, inalenga kukamilisha na kuanzisha ujenzi wa miradi mingine mipya, ikiwamo katika sekta za maendeleo ya elimu, afya, barabara na miundombinu mingine kwenye jamii.

Hiyo kitaifa ni serikali inayoongozwa na Rais Mama Samia Suluhu Hassan, inayolenga kuwanufaisha Watanzania wote katika kila kada na makundi ya kijamii, mtazamo ni kuondoa kero zinazowakabili wananchi hao, ikiwa ni pamoja na kuanzisha miradi mipya ya kimkakati iliyoko katika utekelezaji.

Binafsi namuunga mkono sana Rais, kwa kuona umuhimu huo akachukua hatua za kuhakikisha anapambana ipasavyo akiamini itatoa fursa kila Mtanzania unufaike nayo pindi itakapokamilika kujengwa, akiendeleza nyendo za watangulizi.

Watanzania wenzangu, niseme Rais anajitahidi kuonyesha uwezo alionao wa kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele, hata anapoona watendaji wakienda kinyume na maadili ya utumishi wa umma, anawavurumisha, ili kutimiza azma ya kaulimbiu ya serikali yake 'kazi iendelee.'

Wiki hii mboni yangu ya jicho imejisogeza wilayani Magu mkoani kwetu Mwanza, ambako halmashauri ya wilaya hiyo inakusudia kutenga fedha kwa ajili ya kuunganisha taa za barabarani mitaani ikitumia fedha za makusanyo ya ndani, ili kuwaondolea kero wananchi wake na wageni wao kutoka katika maisha ya kupita gizani nyakati za usiku.

Pia, najua halmashauri hiyo iko katika matarajio ya kutekeleza ujenzi wa stendi mpya ya kisasa ya mabasi mjini humo na stendi ya mabasi madogo, eneo la Kisesa ili kuondoa adha wanayoipata abiria wake wanaposafiri na wale wanaotoa huduma mbalimbali za kijamii katika maeneo hayo.

Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, walitoa mapendekezo hayo katika mkutano wao wa baraza, walipopitisha bajeti yao ya mwaka wa fedha 2022/23 ya shilingi bilioni 50.662, iliyosomwa na Mchumi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Phabian Kabambara.

Wanasema hata miji mingine kama vile Kahangara, Nyanguge na Kisesa nayo itanufaika na taa hizo za barabarani, nami binafsi nawapongeza kuchukua uamuzi huo ili kuwaletea maendeleo wana Magu na vitongoji vyake, hivyo unahitajika usimamizi imara usiolega.

Siku zote mtu anaambiwa kupanga ni kuchagua. Anaweza kuamua, kila kitu ni mipango na uthubutu wa kutekeleza, hivyo nawapa hongera sana Halmashauri ya Magu hususani madiwani kuliona hilo la kukusudia kuujenga Mji wa Magu katika mandhari ya kisasa, ambao utakuwa mfano kwa wilaya nyingine mkoani Mwanza.

Hatua waliofikia ni njema kabisa, isipokuwa angalizo kutoka uzoefu ni tabia za baadhi ya watendaji wasiokuwa waaminifu, ambao mradi unapoibuliwa, wao kazi yao ni kubadilisha matumizi yake bila ya kufuata taratibu, ili kuukwamisha, aweze kupata mwanya wa kufanya ubadhirifu. Hao tuwaogopeni kama ukoma kwenye miradi yetu.

Watendaji wa aina hiyo wana roho za tamaa 'mtakavyote', wahujumu uchumi, wanaotaka kunufaika binafsi badala ya jamii nzima. Nimewahi kushuhudia mradi mmojawapo hapohapo Magu wakati fulani uliokuwa tayari unaendelea, ukatekelezwa kwa kusambazwa mabomba ya maji.

Cha ajabu baada ya siku kadhaa mabomba hayo yalipotea ghafla kumbe mradi ulihamishiwa kata nyingine na wajanja, ambako haukuwa umepangwa kutekelezwa kwenye bajeti, hakuna kiongozi aliyeitisha mkutano wa hadhara wa kata wala kijiji kuelezea wananchi kilichotokea.

Kitendo hicho kilinipa maswali mengi ya kutafakari nakujiuliza kulikoni? Maana mahali hapo sikuwahi kusikia hata ufuatiliaji kutoka baadhi ya viongozi wao wa kuchaguliwa, walau wananchi kufahamishwa hata kama mradi wao umehamishwa.

Nawaambieni baadhi ya watendaji wa kata na watumishi wa aina hii, itakapotokea upotoshaji wa namna yoyote ni ukiukwaji mkubwa wa mali ya umma.

Wenye mamlaka katika maendeleo yetu iwe kwenye kata zenu na vijiji, mitaa au vitongoji. Katika siri yoyote kwenda kinyume na ilivyopangwa rasmi ni ukiukwaji na daima si vinginevyo.

## Madereva waonywa juu ya ukwepaji kulipa kodi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA) mkoani Shinyanga, imewaonya madereva wa bodaboda na bajaji wanaokwepa kulipia leseni za usafirishaji na ada zingine.

LATRA imesema kitendo kinachofanywa na waendeshaji na wamiliki wa vyombo hivyo, kinaikosesha serikali mapato.

Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Shinyanga, Bahati Musiba, alisema hayo juzi kwenye mafunzo ya bodaboda na bajaji Manispaa ya Shinyanga kwa ajili ya kuwajengea uwezo namna ya kufanya biashara zao katika mfumo rasmi na kuzingatia sheria na kanuni za nchi.

Mafunzo hayo yalitolewa na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Alisema asilimia kubwa ya madereva wa bodaboda na bajaji, wamekuwa na tabia ya kutolipia leseni za usafirishaji na ada zingine ambazo zinatolewa na LATRA.

"Naombeni sana madereva wa bodaboda na bajaji mkoani Shinyanga, muwe wazalendo mje mlipie leseni za usafirishaji LATRA.

Msiwe wakwepaji kodi na kuikosesha serikali mapato, msisubiri tuanze kukamatana na kutozana faini. Fedha hizi ambazo mtalipa ndizo zinarudi kwenu wananchi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo," alisema Musiba.

Naye Mkuu wa Usalama Barabarani Wilaya ya Shinyanga (DTO), Dezidery Kaigwa, akizungumza kwenye mafunzo hayo, aliwataka madereva hao wa bodaboda na bajaji, kutii sheria za usalama barabara na kuacha kuendesha mwendokasi hususani kwenye maeneo ya vivuko vya watembea kwa miguu.

Mtaalamu wa Sheria kutoka MKURABITA, Harvey Kombe, alisema wametoa mafunzo hayo ili kuwajengea uwezo madereva wa bodaboda na bajaji katika Manispaa ya Shinyanga.

Baadhi ya madereva hao, walisema wamefurahia kupata mafunzo hayo, huku wakiahidi kutii sheria za usalama barabarani na kuziomba taasisi za fedha kulegeza masharti ili wapate mikopo ya bodaboda na bajaji.

# Serikali yaombwa kuziwezesha asasi hamasa chanjo UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imeombwa kuangalia uwezekano wa kuziwezesha asasi za kiraia, kwa kuzipa fungu maalumu la fedha, ili ziweze kushiriki kikamilifu katika kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kupata chanjo ya UVIKO-19.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu mwenendo wa chanjo ya ugonjwa huo.

"Nimesikia taarifa iliyotolewa na Mganga Mkuu wa Serikali kuwa tangu kuanza kwa chanjo mwaka jana hadi Februari 6, mwaka huu ni watu 2,117,387, sawa na asilimia 3.67 ambao wamechanjwa," alisema Ngawaiya na kuongeza:

"Halafu Mkoa wa Dar es Salaam wenye asasi nyingi za kiraia unatajwa kuongoza kwa idadi kubwa zaidi ya waliothibitika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO-19 ukiwa na wagonjwa wapya 184 kati ya visa vipya 252 vilivyoripotiwa."

Mwenyekiti huyo alisema, hayo yanamfanya aone umuhimu wa kuiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuzipatia fungu la fedha asasi za kiraia ili nazo pia ziingie vitani kuhamasisha wananchi kuchanja.

" Ninaamini kwamba, watu kutojitokeza kwa wingi kuchanja kunatokana na sababu mbalimbali, ikiwamo pia upotoshaji unaofanywa kwa makusudi na baadhi ya watu na pia ukosefu wa elimu kuhusu umuhimu wa chanjo," alisema.

Alisema, zamani asasi za kiraia zilikuwa zikisaidiwa na wafadhili wa nje, na kwamba ufadhili huo umepungua, hivyo anaiomba serikali kuchukua nafasi hiyo ili asasi nazo zitoe mchango katika vita dhidi ya UVIKO-19.

Alisema, serikali ikitenga fungu la fedha na kuzipa asasi za kiraia zinaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha wananchi na kujitokeza kwa wingi kuchanjwa ili kuepuka ugonjwa huo hatari.

"Kwa kuwa mikusanyiko bado imezuiwa, serikali ikitenga fedha na kuzipa asasi hizo, zitapita mitaani kwa magari ya matangazo na kuelimisha wananchi na kuwahamasisha kujitokeza kwa wingi kuchanjwa," alisema.

Alifafanua kuwa ili kufanikisha hilo, zinahitajika fedha ili kukodi magari, vipaza sauti na kununua mafuta, na kwamba ndiyo maana anaomba serikali iangalie uwezekano wa kutenga fungu la fedha ili kufanikisha kampeni hiyo.

Alisema Tanzania ina watu zaidi ya milioni 50, na kwamba kwa muda wa miezi sita tangu chanjo ilipozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa Julani mwaka jana, anaona idadi ya waliochanjwa bado ni ndogo.

"Chanjo ni hiari, lakini ninaamini wapo watu wanahitaji kuchanja, na huenda hawajapata elimu sahihi, na wengine inawezekana wanazuiwa, hivyo ni vyema asasi za kiraia zikaingia mitaani kusaidia kuweka mambo sawa," alisema.

Ngawaiya alisema, asasi za kiraia zina umuhimu wake kwa maendeleo ya taifa, na kwamba ni muhimu zikashirikishwa kikamilifu kwa kutengewa fungu la fedha kwenye suala la kuhimiza chanjo ya UVIKO-19.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi cha Benki ya CRDB, Stephen Adili (kushoto) na Meneja wa Benki hiyo, Tawi la Azikiwe, Hamis Saleh (kulia), wakifurahia jambo, baada ya kukabidhi zawadi kwa washindi wa BSS 2021, Yohana Braison Mwayinga (mshindi wa kwanza), Andrew Charles Magalata (mshindi wa pili), Suleiya Abdi Abdillah (mshindi wa tatu), jijini Dar es Salaam jana. Watatu kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya BenchMark ambao ndio waendeshaji wa mashindano ya BSS, Ritha Paulsen. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uwekezaji utalii maeneo mengine wapendekezwa

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Viti Maalum kutoka Zanzibar, Asya Mwadini Mohammed, ameishauri serikali kuwekeza katika eneo lingine la utalii hasa mambo ya kale badala ya wanyamapori pekee.

Alisema hayo jana wakati akichangia ripoti ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ya Bunge, jijini Dodoma.

Alisema utalii wa wanyamapori unaiingizia serikali mapato mengi, lakini kuna sekta nyingine hazijaguswa ambazo kama zitapewa kipaumbele mapato yanatongezeka.

Mbali ya utalii huo, pia alipendekeza mkazo uwekwe katika utalii wa fukwe, utamaduni na utalii wa nyuki.

Alisema hizo ni sekta ambazo wanawake wanaweza kuziendesha kujiingiza mapato, huku serikali pia ikiongeza mapato yake.

Mbunge huyo alisema kama serikali inahofia gharama kuwekeza katika sekta hizo, inaweza kuwashirikisha wawekezaji wa ndani na nje.

Kuhusu uandaaji wa sera za utalii, aliishauri wizara husika kukutana na taasisi nyingine ili kupunguza migongano hasa kwa kuzingatia sekta hiyo ni mtambuka.

Mbunge huyo alisema masoko ya utalii yaliyoko hayaridhishi na kuishauri mamlaka iliyopewa jukumu la kusimamia sekta hiyo kuongeza kasi ya kutangaza vivituo ili kuongeza watalii na uwekezaji katika sekta hiyo.

Awali akiuliza swali kuhusu mkakati wa serikali kudhibiti uchafuzi mazingira katika fukwe za bahari, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, alisema wizara imetoa miongozo ya jinsi ya kuzichakata taka zote zinakwenda baharini ili kupunguza uharibifu.

Hata hivyo, alisema baadhi ya taka kama vibati vya soda ni vigumu kuchakatwa, lakini serikali imejizatiti kuendelea na kampeni ya usafi katika fukwe zote za bahari.

# Tanzania yaiunga mkono hifadhi Ziwa Tanganyika

**Na Benny Mwaipaja,** DODOMA

TANZANIA imeahidi kuunga mkono utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Kikanda ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika kutokana na umuhimu wake kwa wananchi wa nchi nne zinazonufaika nayo.

Nchi hizo ni Tanzania, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia Congo, Rwanda na Zambia.

Ahadi hiyo ilitolewa jijini Dodoma na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alipokutana na kufanya mazungumzo na Ujumbe wa Sekretarieti ya Mamlaka ya Ziwa Tanganyika (LTA) uliofika ofisini kwake kuomba idhini ya serikali ya kuanza kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Tutuba alisema serikali inaunga mkono kuanza kwa Awamu ya Pili ya Programu ya Kikanda ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika (PRODAP II) baada ya Awamu ya kwanza ya program hiyo iliyokamilika mwaka 2014 kuwa na manufaa makubwa kwa wananchi wanaozunguka Bonde la Ziwa Tanganyika katika nchi hizo nne za kikanda.

"Katika kuandaa mradi wa awamu ya pili tumekubaliana kuwa sisi kama Wizara ya Fedha na Mipango tutaratibu wizara nyingine ili tupate vipaumbele ambavyo tutaviwasilisha katika Taasisi yake ili iweze kuviunganisha na vile vya nchi wanachama kisha kuiwasilisha katika Benki ya Maendeleo ya Afrika ili waweze kufanya upembuzi yakinifu ili miradi hiyo ikitekelezwa iweze kuwiana na malengo ya kupunguza umasikini kwenye jamii inayozunguka eneo hilo" alisema Tutuba.

Alisema kuwa katika Awamu ya kwanza, Mamlaka ya Hifadhi ya Ziwa Tanganyika ilitekeleza mradi wa ujenzi wa masoko eneo la Kibirizi mkoani Kigoma ambapo wameweka vifaa mbalimbali vya uhifadhi wa samaki na dagaa, maeneo ya kukaushia samaki na maghala ya kuhifadhia samaki.

Tutuba alisema miradi mingine iliyotekelezwa ni ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule 22, vyoo kwenye shule 18, miradi mitano ya vituo vya afya, nyumba za watumishi kwenye vijiji viwili na zahanati moja na miradi 10 ya maji katika vijiji vinavyozunguka Ziwa Tanganyika.

Miradi mingine ni ujenzi wa kilomita 65.6 za barabara, madaraja mawili na kufanya kampeni 180 za kujikinga na magonjwa ya kuambukiza ukiwamo Ukimwi.

Aidha, alisema kuwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa programu hiyo, Tanzania imekuwa ikichangia kila mwaka dola 303,900 ambapo kiwango hicho kinachangiwa na kila nchi mwanachama na kwamba miradi hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi na kupunguza umaskini kwa wananchi.

Alisema kuwa Tanzania iko tayari kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu hiyo kutokana na fedha zitakazopatikana kwa njia ya mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa kuwa miradi iliyotekelezwa kupitia ushirikiano huo imeleta maendeleo uendelevu wa mazingira katika Ziwa Tanganyika na inagusa sekta mbalimbali za kuondoa umaskini kwa wananchi.

Naye Balozi wa Tanzania nchini Burundi, ambaye anasimamia maslahi ya Tanzania katika Sekretarieti ya Mamlaka ya Ziwa Tanganyika yenye makao yake makuu nchini Burundi, Dk. Jilly Maleko, alisema lengo la ziara ya sekretarieti hiyo nchini ni kufanya mazungumzo kuhusu uwezekano wa kupata mkopo kutoka AfDB kwa ajili ya kutekeleza awamu ya pili ya programu hiyo.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Mwanga Hakika, Muhandisi Ridhuan Mringo (kulia), akikabidhi msaada wa meza na viti 474 vyenye thamani ya Sh. milioni 30 kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mwanga, Mwajuma Nasombe, kwa ajili ya Shule za Sekondari wilayani humo. Anayeshuhudia mwenye kaunda suti ya buluu ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Abdallah Mwaipaya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yamwaga madawati ya mil. 472/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Mwanga Hakika, imetoa madawati na meza 472 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 30 kwa shule za sekondari wilayani Mwanga ili kukabiliana na uhaba wa samani hizo.

Vifaa hivyo vitasaidia kupunguza uhaba wa viti na meza kwa wanafunzi wapatao 13,429 kutokana na ongezeko la wanafunzi 233 kwa mwaka wa masomo 2021/22.

Kabla ya msaada huo, wilaya hiyo ilikuwa na upungufu wa viti na meza 689 kwenye shule 10 kati ya 26 za sekondari.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Mwanga Hakika, Mhandisi Ridhuan Mringo, alisema lengo la msaada huo ni kuunga mkono jitihada za serikali kuhakikisha wanafunzi wanakuwa katika mazingira bora ya kujifunzia.

"Benki yetu inatekeleza sera yake ya wajibu kwa jamii kwa kuangalia maeneo yenye uhitaji ikiwamo sekta ya elimu.Msaada huu wa madawati ni katika kuhakikisha wanafunzi wanapata mazingira bora ya kujifunzia pamoja na kuunga mkono jitihada za serikali katika kukuza sekta ya elimu hapa nchini," alisema Mringo.

Alisema benki hiyo itaendelea kuunga mkono jitihada za maendeleo ili kuhakikisha malengo makubwa ya taifa yanafikiwa kwa asilimia kubwa.

"Benki yetu imeweza kukua kutoka kuwa benki ndogo na kuwa benki inayokuwa kwa kasi.Tunaamini ukuaji wa benki hii unatupa uwezo wa kuweza kuchangia zaidi kwenye masuala ya kijamii kama ilivyofanyika hii leo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya, aliishukuru Benki ya Mwanga Hakika kwa kuwa mshirika mkubwa wa maendeleo wilayani humo na kwamba itasaidia kufanikisha mipango mikubwa ambayo Wilaya hiyo imejiwekea kwa mwaka 2021/22.

"Madawati haya yanakwenda kwenye shule ambazo tulikuwa tuna upungufu mkubwa wa zaidi ya madawati 600. Kwa ujumla tunashukuru kwa madawati haya yatamaliza matatizo ya madawati kwenye shule za sekondari na baadaye tutageukia shule za msingi," alisema. Mbali na msaada huo, wilaya hiyo imejenga madarasa 50 katika shule za sekondari ikitumia Sh. milioni 976 kutoka vyanzo mbalimbali ikiwamo bajeti kuu Sh. milioni 500, fedha za UVIKO-19 Sh. milioni 200, fedha za ndani Dh. Milioni 30 na fedha za EP4R Sh. milioni 237.

## Mwalimu wa dini mbaroni tuhuma kuwalawiti watoto

**Na Neema Hussein,** MPANDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi linamshikilia Joseph Paulo (27) ambaye ni mwalimu wa mafunzo ya Komunio ya Kwanza katika Kanisa Katoliki Jimbo la Mpanda kwa tuhuma za kulawiti watoto.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Hamad, alisema jana kuwa mtuhumiwa alikuwa akiwalaghai watoto hao kwa kuwabeba kwenye pikipiki yake.

Hamad alisema mbali na kuwabeba kwenye pikipiki, alikuwa akiwaambia wamsindikize kwenye shughuli zake za kibiashara.

Alisema baada ya kumaliza vipindi vyao vya masomo, alikuwa akiwafanyia vitendo hivyo vya kikatili kwa nyakati tofauti na maeneo mbalimbali.

Kamanda Hamad alisema mtoto anapofanyiwa vitendo hivyo hupata madhara ya kisaikolojia, kimwili na akili.

Alisema wakati wakifanya upelelezi baada ya kuwauliza watoto hao (majina yamehifadhiwa) walikiri kufanyiwa vitendo hivyo na mtuhumiwa alikiri kuwafanyia.

Kamanda Hamad alisema mtuhumiwa amefikishwa mahakamani na upelelezi wa shauri hilo umekamilika.

**Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Hamad, alisema jana kuwa mtuhumiwa alikuwa akiwalaghai watoto hao kwa kuwabeba kwenye pikipiki yake. Hamad alisema mbali na kuwabeba kwenye pikipiki, alikuwa akiwaambia wamsindikize kwenye shughuli zake za kibiashara.**

## Mpoto apewa nguvu ya kutangaza miradi

Na Romana Mallya

KAMPUNI ya JATU PLC inayojishughulisha na kilimo imemteua msanii wa muziki, Mrisho Mpoto, 'Mjomba' kuwa balozi wa miaka mitatu wa kampuni hiyo ili kutangaza miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali.

Februari 7, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alimteua msanii huo kuwa balozi wa sekta ya maji baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kusifu umahiri wake wa kukariri gharama za miradi ya maji na kuzitamka, wakati wa hafla ya uwekaji jiwe la msingi katika mradi wa maji wa Bunda mkoani Mara.

Akizungumza juzi mkoani Dar es Salaam, Meneja Mkuu wa Kampuni ya JATU PLC, Mohamed Simbano, alisema kwa kutambua kazi kubwa inayofanywa na serikali kampuni yao imeamua kumuunga mkono Rais Samia kwa kumpa ubalozi msanii huyo kwa kipindi hicho.

Simbano alisema mbali ya ubalozi huo, wamemwandalia kipindi maalum kijulikanacho, 'Kaa hapa awamu ya pili' kwa ajili ya kuendelea kuitangaza miradi ya maendeleo ya serikali.

"Baada ya serikali kumteua Mpoto kuwa balozi wa maji kwa kutambua umuhimu wa maji katika sekta ya kilimo JATU PLC imeona iunge mkono juhudi za maendeleo zinazofanywa na serikali kwa kumpa mkataba wa miaka mitatu ili atangaze shughuli za maendeleo.

Alisema sekta ya maji ni nguzo muhimu katika kuleta mapinduzi ya kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji ambacho hufanywa mikoa mbalimbali.

"Katika kipindi cha miaka mitano JATU PLC imeingiza kampuni katika soko la hisa la DSE, kufungua ofisi kikanda ndani ya nchi na Afrika Mashariki kwa kuanza na Kenya kwa ajili ya kupanua wigo wa masoko ya ndani na nje, kufungua kampuni ya Bima ya Kilimo na Ufugaji. Ongezeko la wakulima zaidi ya 5,000, kutoa ajira rasmi 500 na zisizo rasmi zaidi ya 10,000," alisema.

Baada ya kusaini mkataba na kampuni hiyo, Mpoto aliahidi kutangaza mambo mazuri yanayofanywa na serikali chini ya Rais Samia.

"Katika fedha za Uviko-19, serikali imetenga asilimia 10 ya fedha zote sawa na Sh. bilioni 139.8 ambazo zimepelekwa sekta ya maji ambayo ndiyo sekta pekee iliyopewa fedha nyingi. Najua Watanzania wengi hawajui hili, hii ndiyo kazi yangu ya kuwaelimisha," alisema.

Alisema yapo mambo makubwa ambayo yamefanywa chini ya Rais Samia lakini hayasimuliwi hivyo moja ya kazi kubwa anayokwenda kuifanya ni kuwaeleza Watanzania.

"Ninaishukuru serikali kwa kuniteua kuwa balozi wa sekta ya maji na uteuzi huo umefanya leo (juzi) JATU PLC mkaniteua kwa mara nyingine kuwa balozi wenu kwa mkataba mkubwa wenye heshima kubwa, nawahidi sitawaangusha," alisema.

# Chakula bora shida kwa wajawazito wa Kigoma

**Na Deogratius Nsokolo,** KIGOMA

ZAIDI ya asilimia 60 ya wajawazito wanaofika kujifungua katika vituo vya kutolea huduma katika mkoa wa Kigoma hukutwa na upungufu wa damu unaosababishwa na kutokula vyakula bora katika ngazi ya familia.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Dk. Simon Chacha, alisema hayo wakati Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa FAO likikabidhi vifaa vya mawasiliano kwa idara ya afya mkoa kuwa utafiti unaonyesha kuwa akinamama wengi wajawazito wanaofika hospitali kwa ajili ya kujifungua wanakutwa na upungufu wa damu.

Alisema hali hiyo inatokana na kutokula mlo kamili wakiwa nyumbani hali ambayo imekuwa ikisababisha ongezeko la vifo kutokana na uzazi na kwamba watavitumia vifaa hivyo ambavyo ni seti ya televisheni 16 na kompyuta mpakato kutoa elimu kwa jamii kuhusu lishe ili kupunguza udumavu na utapiamlo.

Akikabidhi vifaa hivyo Mwakilishi msaidizi wa Shirika hilo nchini Charles Tulahim alisema utaoji wa vifaa hivyo unalenga kutekeleza malengo ya milenia pamoja na lengo la Mkoa wa Kigoma kupunguza udumavu na utapiamlo kwa kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa jamii na hasa kwa wanawake.

Alisema shirika hilo ambalo linafadhili miradi mbalimbali ya kilimo na chakula mkoani Kigoma, litaendelea kushirikiana na serikali katika kuhakikisha teknolojia ya lishe inapata kipaumbele na familia zinaanza kula mlo kamili ili kusaidia kupunguza magonjwa yasiyo ya lazima, ambayo husababishwa na ukosefu wa vitamini mwilini.

Tulahi alisema ulaji wa mboga na matunda bado uko chini na vifaa hivyo vya mawasiliano vitakwenda kusaidia kuonyesha namna tofauti ya uandaaji wa vyakula katika jamii.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma, Rashid Mchatta, alisema televisheni hizo zitapelekwa katika vituo vya afya katika wilaya zote ambako ujumbe kuhusu lishe utakuwa ukitolewa mara kwa mara kwa watu wote wanaofika kwa ajili ya ujumbe mbalimbali.

Kutokana na hali ya udumavu na utapiamlo, Mchatta aliwataka wazazi kutowaacha watoto peke yao nyumbani badala yake wazingatie malezi bora ili watoto waweze kukua vizuri.

"Tatizo kubwa tunalokabiliana nalo katika mkoa wetu ni wazazi kuwaacha watoto waleane wenyewe, wazazi wanasafiri na kwenda kuishi mashambani, huku wanabaki watoto ambao hawajui kubadilisha chakula, wanabaki, wanakula chakula cha aina moja kila siku hali ambayo inachangia matatizo ya kiafya kwa watoto wengi na watu wazima", alisema Mchatta.

Kwa mujibu wa Mchatta, Mkoa wa Kigoma una chakula kingi na kinachotosheleza mahitaji, ila tatizo ni mpangilio wa chakula katika ngazi ya familia ambao hauzingatii uwiano.




Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo (mwenye shati la buluu), akipokea sehemu ya msaada wa mabati 222, mbao 454 na vifaa vingine vya kuezekea madarasa kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, vilivyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya kusaidia shule mbili za msingi za Keko Magurumbasi na Buza, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Neema ya maji kwa wawekezaji viwandani yaja

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAWEKEZAJI wa viwanda katika eneo la Zegereni wilayani Kibaha mkoani Pwani hivi karibuni wataondokana na kikwazo cha ukosefu wa maji kutokana na mradi wa maji ambao umeanza kutekelezwa katika eneo hilo.

Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salam (DAWASA) Kibaha, Alpha Ambokile, alisema mradi huo wa Zegereni ulianza kutekelezwa Novemba 2021 kwa fedha za ndani.

Akizungumza na Nipashe jana mjini Kibaha, alisema mradi huo hadi kukamilika utagharimu Sh. bilioni 2.5.

Ambokile alisema mradi huo ukikamilika utaondoa kero ya maji katika eneo hilo la viwanda pamoja na wananchi wa mitaa ya Jonnung'a, Saeni na Zegereni.

Alisema mradi huo ambao umefikia asilimia 41 za utekelezaji wake ni kati ya miradi ya mikakati miwili inayotekelezwa kwenye eneo lake la Kibaha. "Malengo yetu mradi huu ukamikike mwishoni mwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, lakini kwa kuwa tunategemea fedha za ndani itategemea upatikanaji wa fedha hizo," alisema.

Kwa mujibu wa Ambokile, mradi mwingine mkubwa wa kimkakati utatekelezwa katika Kata ya Pangani utatumia fedha za ndani na utagharimu Sh. bilioni 7.4 hadi kukamilika.

Alisema mradi huo haujaanza kutekelezwa na kazi yake itakapofanyika utawanufaisha wakazi wa Lulanzi, Pangani, Muheza, Vikawe, kwenye machinjio ya Pangani. Alieleza kuwa ipo miradi mingine midogo midogo ambayo inaendelea kutekelezwa katika eneo lake inayolenga kusogeza huduma karibu na wananchi.

Ambokile alieleza vikwazo wanaokabiliana navyo katika utekelezaji wa miradi hiyo ni wananchi kutoridhia kuruhusu mabomba kupita katika maeneo yao na kutotunza miundombinu ya mabomba baada ya kulazwa.

# Ataka vifaa vya maabara shuleni

MBUNGE wa Temeke (CCM), Dorothy Kilave ameibana serikali kumaliza tatizo la uhaba wa vifaa vya maabara kwenye shule za sekondari ili wanafunzi wasikwepe masomo ya sayansi.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alihoji lini serikali itaajiri Walimu wa sayansi katika shule za sekondari za Kata katika Wilaya ya Temeke.

"Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo kubwa la uhaba wa vifaa vya maabara ambalo linasababisha wanafunzi kukwepa masomo ya sayansi?,"alihoji.

Katika majibu ya Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ilisema katika mwaka wa fedha 2020/21 ilinunua na kusambaza vifaa vya maabara katika shule za sekondari za kata 1,258 nchini zikiwamo 12 Manispaa ya Temeke ili kuwafanya wanafunzi kujifunza kwa vitendo masomo ya sayansi.

Ilisema kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ya Elimu nchi itaendelea kununua na kusambaza shuleni vifaa vya maabara katika shule za sekondari nchini.

Aidha, ilisema kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 iliajiri Walimu 6,949 ambapo kati yao asilimia 79 walikuwa walimu wa sayansi.

Ilisema walimu hao walipangiwa vituo katika shule za sekondari za Serikali kipaumbele kikiwa ni shule zenye upungufu mkubwa kulingana na mahitaji ya wakati huo.

Hata hivyo, ilisema imefanya tathmini ya mahitaji ya walimu wa sayansi katika shule za Sekondari na kubaini kuwa Manispaa ya Temeke ina upungufu wa Walimu wa Sayansi 706 sawa na asilimia 73.3 ya mahitaji.

Ilisema serikali itaendelea kuajiri walimu wa fani zote na kuwapangia vituo kulingana na mahitaji ya Shule za Sekondari zote nchini, zikiwemo Shule za Sekondari za Manispaa hiyo.



Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, akichangia kuhusu taarifa ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mwaka 2021, iliyowasilishwa Bungeni, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Benki ya Convenant yaendelea kufilisiwa

BUNGE limeelezwa kuwa Bodi ya Bima ya Amana inaendelea na ufilisi wa Benki ya Convenant kwa kukusanya mali na madeni ili kupata fedha za kuwalipa wateja waliokuwa na amana zinazozidi Sh.milioni 1.5.

Wizara ya Fedha na Mipango, ilitoa kauli hiyo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Tandahimba (CCM), Katani Katani.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini Serikali itawalipa wakulima wa korosho fedha zao walizofanya biashara msimu wa 2017/18 na iliyokuwa Benki ya Covenant iliyofungwa kabla ya wakulima hawajatoa fedha zao.

Katika majibu yake, Wizara hiyo ilisema kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufilisi kiasi kitakacholipwa kitategemea fedha zitakazopatikana kutokana na kuuza mali za benki hiyo.

Ilifafanua kuwa Benki Kuu ya Tanzania ilifutia leseni iliyokuwa Benki hiyo Januari 4, Mwaka 2018 kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006.

Ilisema baada ya kuifutia leseni, Benki Kuu iliiteua Bodi ya Bima ya Amana kuwa mfilisi wa Benki hiyo kwa mujibu wa sheria.

Ilibainisha kuanzia mwezi Machi 2018, Bodi ya Bima ya Amana ilianza zoezi la kulipa fidia ya Bima ya Amana ya kiasi kisichozidi Sh.milioni 1.5 kwa wateja waliostahili kulipwa Bima ya Amana wakiwamo Wakulima wa Korosho wa Wilaya ya Tandahimba na zoezi hilo bado linaendelea kwa wateja ambao hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.

Kwa mujibu wa Wizara, hadi kufikia mwezi Desemba 2021, jumla ya Sh.milioni 332.71 zimeshalipwa kwa Wakulima wa Korosho 1,078 kati ya Wakulima 1,346 wa Wilaya ya Tandahimba waliokuwa na amana katika Benki hiyo.

Ilisema kiasi hicho ni sawa na asilimia 98 ya kiasi cha Sh.milioni 337.99 zilizotengwa kwa ajili ya kulipa fidia katika kituo cha Tandahimba.




Habari zote na Augusta Njoji

## Mabwawa h/shauri kufanyiwa tathmini

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ina mpango endelevu wa kufanya tathmini ya mabwawa yaliyopo katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Wizara hiyo ilibainisha hayo bungeni jana katika majibu yake kwenye swali la Mbunge wa Mikumi (CCM), Dennis Londo.

Katika swali lake, Londo alitaka kujua mpango wa serikali wa kuhakikisha Bwawa la Zombo linatumika kikamilifu kwa ufugaji wa samaki na kuongeza ajira kwa vijana.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema tathmini hiyo inafanyika ili kufahamu uwekezaji unaofaa kwenye bwawa husika kulingana na jiografia ya eneo hilo.

Aidha, ilisema kwa kuwa shughuli hiyo ni endelevu na hufanyika kwa awamu, Bwawa la Zombo litaingia kwenye mpango wa tathmini katika mwaka wa fedha 2022/23 ili kujua aina ya uwekezaji unaofaa katika bwawa hilo.

Vile vile, ilisema wataalamu wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira – Morogoro kitatoa mafunzo maalumu ya ufugaji samaki kwa vijana wa Mikumi ili kuwapa stadi za ufugaji samaki wenye tija kwenye mabwawa.

## 'Polisi inatosha usimamizi wa kampuni ulinzi'

SERIKALI imesema haioni sababu ya kuanzisha chombo maalumu cha kuzisimamia kampuni binafsi za ulinzi na kusisitiza kuwa Jeshi la Polisi linatosha kufanya shughuli hiyo.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilitoa kauli hiyo bungeni jana katika swali la Mbunge wa Pangawe, (CCM), Haji Amour Haji.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali haioni haja ya kuwepo kwa chombo hicho kitakachozisimamia shughuli zote za kampuni hizo ili kuongeza wigo wa kiutendaji.


"Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwepo kwa sheria itakayosimamia kampuni binafsi za ulinzi ili kuongeza ufanisi?,"alihoji.

Katika majibu yake, Wizara ilisema Jeshi la Polisi linatosha kusimamia shughuli za kampuni hizo kama ilivyo sasa kwa sababu ndiyo taasisi iliyopewa mamlaka kisheria ya kutoa leseni na hati za umiliki wa silaha hapa nchini ambazo pia humilikiwa na kampuni hizo.

Ilisema utaratibu huo hutoa urahisi wa kufuatilia mwenendo wa makampuni katika utunzaji na matumizi ya silaha hizo.

Hata hivyo, ilisema serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa sheria itakayosimamia kampuni hizo na tayari mapendekezo ya kutungwa kwa sheria yapo kwenye hatua ya awali za mawasiliano baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Ilisema baada ya maridhiano kati ya serikali hizo kufikiwa, maandalizi ya Sheria hiyo yataendelea kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.




Ukurasa 13

kurasa 12

## Wakala mbegu wajitosa kuzalisha alizeti, michikichi kunusuru uhaba



BUFE
Ijumaa Februari 11, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

BIASHARA

# Mkufunzi NCT Dk. Divecha: Mhudumu hoteli silaha kuu milango 5 ya fahamu

- Unadhifu, tabasamu, ukarimu, lugha kadhaa...
- Mgahawa wake balaa!...akampikia Rais Mwinyi
- Ugali aliopika Nairobi ukampa 'scholarship' nje

**Na Christina Mwakangale**

UMEWAHI kufikiri kwamba katika shughuli zako za kibiashara na zinazokuunganisha wewe pamoja na wateja kwamba, zinahusiana na milango ya fahamu?

Binadamu ana milango mitano ya fahamu; masikio, ulimi, macho, ngozi na pua, vikitajwa kuwa na uhusiano mkubwa na mbinu za kumteka mteja katika biashara.

Mkufunzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), Dk. Milan Divecha, anasema kati ya makosa yanayofanyika kwenye biashara ni kutoitumia milango hiyo ya fahamu, ambayo kila moja ina kazi yake.

Mwanazuoni huyo wa masuala ya hoteli zaidi ya miaka 30, anatoa siri ya kufanikiwa kufanya biashara hasa ya mapishi katika hoteli na migahawa, wakati wa kongamano la kuelekea mahafali ya 19 ya NCT, jijini Dar es Salaam, hivi karibuni.

Hapo wamehitimu wasomi wa mafunzo ya ukarimu, mapishi, uhudumu chakula na vinywaji, utunzaji vyumba, kufua, uongozi na usafirishaji watalii, uratibu matukio na mapokezi kwa ngazi ya astashahada na stashahada.

Dk. Divecha anasema mteja anapofika kwenye biashara, iwe hoteli au mgahawa, mtoa huduma amsikilize kwa makini hapo anafafanua:"Tumia sikio kusikia sahani inapolia chakula kimeisha, toa sahani au mteja ataongeza.




Mkufunzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT), Dk. Milan Divecha.
**PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

"Tumia tabasamu, tazama kila kitu alipo mteja wako sio unamtelekeza meza haina chochote au imepungua kitu fulani hadi aanze kukutafuta kukuita. Inaleta usumbufu na kesho asirudi, 'customer care' ni kitu kikubwa.

"Mteja anapofika hotelini kwako unatakiwa kumsikiliza kwa masikio yako. Tuna milango mitano ya fahamu, mitano ambayo inatumika katika 'customer service'. Kwenye utafiti tumebaini watu wanaangalia, lakini hawasikilizi wanayotakiwa kufanya.

"Kwa mwonekano (mhudumu) unaonekana kuvutia, unapendeza hata kufanya mazungumzo na mteja upo vizuri. Lakini, kumpokea mgeni unafahamu?," anahoji Divecha.

"Mteja amekuja kwenye hoteli yako, amekaa na kuagiza chakula? Unatakiwa kumsikiliza na kumpatia chakula muda muafaka na hakikisha kuna kila kitu kwenye meza aliyokaa. Sio mara chumvi imekosekana au haitoki, uma, kisu hakuna. Umempokea vizuri na chakula kapata ndani ya muda, je meza yako imekamilika?"

**MGAHAWANI KWAKE**

Anasimulia kilichojiri katika mgahawa wa kwanza aliouanzisha mkoani Dar es Salaam, akisema: "Mgahawa niliouanzisha na kuwa na hadhi ya juu mtaa wa Samora (Alcove Restaurant) ilikuwa 'Project' yangu ya Masters'(Utafiti Shahada ya Uzamili). Nilifikiria kubadili aina ya shughuli za kifamilia, sababu, mtoto mhandisi mama mhasibu, fikiria ningewezaje.

"Nilipohitimu National Service (JKT) nilipata fursa ya kazi Nairobi (Kenya) kama 'entern'() mahali fulani, kwa sababu nilikuwa najua kupika chakula na kile nilichojifunza nikiwa shuleni, hasa kupika ugali, maharage, mchicha na nyama ya kuchoma nilijikita hapo hapo.

"Kule Nairobi kukiwa na kongamno au wakihitaji 'catering' walikuwa wakihitaji chakula na nilipika, wakaanza kuniulizia kwenye kila hafla. Chakula cha watu 25 nilimudu kukipika vizuri tu, hii ilinifanya kupata 'scholarship' Uswisi," anasema Dk.Divecha.

Inaendelea Uk.12

## UHABA MAFUTA KUPIKA...

# Wakala mbegu wajitosa kuzalisha alizeti, michikichi kunusuru uhaba

## • Mamia hekta shamba la mbegu laandaliwa

**Na Boniface Gideon, MKINGA**

NCHINI hivi sasa kunatajwa kuwapo uhaba wa mafuta ya kupikia. Kuna sehemu kubwa inaagizwa kutoka nje ya nchi, kuziba pengo la mahitaji kitaifa.

Hiyo imeenda mbali, serikali sasa imeingilia kati na mpango mkakati kutaka kuinua uzalishaji wa mafuta ya kula ndani ya nchi na hatua zimeshaanza kuchukuliwa kujitosheleza, vikosi vya ulinzi na usalama kama vile Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Wakala wa Mbegu za Kilimo Tanzania (ASA) chini ya Wizara ya Kilimo, ipo kwenye mikakati ya kuhakikisha upungufu wa mafuta ya kupikia unapungua nchini, huku baadhi ya mikakati hiyo ikiwa ni kuongeza kilimo cha michikichi na alizeti, yote yakiwa mazao mkakati ya kuzalisha mafuta.

Inaelezwa serikali inatumia fedha zaidi ya shilingi nusu trilioni kila mwaka ikiagiza mafuta ya kupikia kutoka nje ya nchi, hivyo azma ya kuinua uzalishaji nyumbani ni namna itakayosaidia kupunguza gharama kubwa, ambazo taifa linatumia kuagiza mafuta kutoka nje.

Mkurugenzi wa Uzalishaji Mazao kutoka ASA, Dk. Justin Ringo, anasema lipo Shamba la Uzalishaji Mbegu Mwele lililopo eneo la Maramba wilayani Mkinga, Tanga lenye ukubwa wa zaidi ya hekta 978 litakalopandwa na kusaidia kupunguza uhaba wa mafuta kitaifa.

Anataja kuwapo maeneo mengine makubwa ya kuzalisha alizeti, mkurugenzi huyo ana ufafanuzi: "Lengo kubwa ni kwenda sambamba na msisitizo wa serikali kuhakikisha mafuta yanapatikana nchini kwa kupatikana mbegu bora za alizeti na michikichi."

Ringo anasema wao kama taasisi ya umma wana wajibu wa kuzalisha mbegu hata za mazao mengine, michikichi na alizeti ikibaki kuwa kipaumbele, lengo la msimu uliopo ni kuzalisha miche ya mbegu 800,000.

"Tunatarajia kusambaza Miche 500,000 na kuzalisha miche 800,000 kwenye msimu huu, lakini pia tunatoa kwa wananchi pamoja na taasisi mbalimbali," anasitiza.

Pia, anafafanua imani yake kwamba iwapo kutawekwa juhudi zaidi ya kuzalisha mbegu na upandaji wa michikichi na alizeti nchini, iko bayana tatizo la upungufu wa mafuta ya kupikia litatoweka.

Anasifu kilimo cha zao la michikichi ni rahisi, pia analitaja kuwa zao rafiki mkubwa wa mazingira, hivyo mkulima ana uwezo wa kuvuna mara nne kwa mwaka.

"Michikichi inasaidia sana kwenye utunzaji wa mazingira hususani vyanzo vya maji. Kwa hiyo, mwananchi au taasisi inaweza ikapanda kama miti ya kusaidia kutunza vyanzo vya maji na mazingira." anaeleza.

Pia, anafafanua faida: "Lakini hapo hapo ukapata na faida za kipato, hivyo ni zao zuri lisilo na gharama kwa mkulima na uvunaji wake ni mara nne kwa mwaka."

Dk. Ringo anasema kutokana na shughuli mbalimbali shambani Mwele, wameshazalisha ajira zaidi ya 500 na miradi mingine kadhaa inayoendana na kilimo hicho.

"Tunaendelea kuongeza wigo wetu na sasa tunamalizia ujenzi wa ghala la kuhifadhi nafaka ambalo limefikia asilimia 90 na msimu huu tutapanda hekta 300 za alizeti, mahindi hekta 90, ufuta hekta tano na kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wanaotuzunguka, ili wapande mazao haya kuongeza kipato," anasisitiza Dk. Ringo



Mkuu wa Wilaya ya Mkinga Mkoa wa Tanga Kanali Maulid Surumbu ( kulia), akimkabidhi mche wa mchikichi Mkuu wa Kitengo Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam DAWASA, Modester Mushi, kwa ajili ya kupanda kwenye ukingo wa Mto Ruvu.



Wadau wa Kilimo wilaya ya Mkinga Mkoa wa Tanga, wakitazama moja ya chanzo cha maji kinachotunzwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo Nchini ASA, kwenye Shamba la Mwele. **PICHA ZOTE: BONIFACE GIDEON.**

### WADAU WA MRADI

Mkuu wa Kitengo cha Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa) Mhandisi Modester Mushi, anasema pamoja na wao kutoa huduma za maji safi, pia usafi wa mazingira wanatumia maji kwenye vyanzo vya mito, lengo linaanzia Mto Ruvu unaowapatia maji zaidi ya asilimia 92, huduma inayotolewa katika mikoa miwili, Dar es Salaam na Pwani.

Anasema wameamua kuchukua miche hiyo ya michikichi 30,000 wakitaka kuzalisha mafuta nchini na wameona ni zao litakalosaidia kutunza vyanzo vya maji.

Kwa mujibu wa Mhandisi Modester, kingo za Mito kwa hivi sasa zinaathirika kwa shughuli za binadamu ikiwamo kilimo na ufugaji, ambazo ni shughuli za kiuchumi za umma.

"Mwananchi badala ya kupanda mazao ya muda mfupi, kupitia michikichi ataweza kuvuna mara nne kwa mwaka na atakuwa mmojawapo anaechangia hatua na jitihada za serikali katika kutengeneza mafuta na kipato chake kitabadilika," anasema Modester

Anatetea upandaji miche kwamba inapokuwa pembezoni mwa mto, inasaidia kupunguza kila shughuli zinazohusisha kugusa ardhi kulimwa, huku kiasi kikubwa cha tope au mchanga kikipungua.

### SERIKALI MKINGA

Mkuu wa Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga, Kanali Maulid Surumbu, anasema mara nyingi Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, amekuwa akihamasisha michikichi izalishwe kwa wingi kitaifa na nchi iondokane na tatizo la mafuta ya kupikia.

Kanali Surumbu anawataka wananchi wa eneo lake kuwekea mkazo zao hilo la michikichi, kwa kuwa hata wilaya inastawi vizuri, hivyo watumie fursa ya kuwapo shamba la Mwele, ambalo limepewa jukumu kuzalisha michikichi kutoa mbegu kwa wananchi.

Anasema hadi sasa wana mashamba mengi yanayomilikiwa na taasisi, halmashauri na watu binafsi, ambayo yakitumika vizuri kuzalisha michikichi wahusika wanakuwa miongoni mwa watu wenye mchango wa kupunguza gharama zinazoingia serikali kuagiza mafuta nje ya nchi.

"Serikali ya wilaya ya Mkinga imejipanga kuboresha na kumsaidia Mkulima asikwame kwa chochote katika azma yake ya kulima zao hilo na mazao mengine, hivyo nitumie fursa hii kuwahamasisha wakulima na wananchi kutilia mkazo kilimo hiki.

"Hii itatusaidia sana kuongeza kipato na kuondoa utegemezi wa mafuta ya kupikia nchini kutoka kwa mataifa ya nje," anahitimisha Kanali Surumbu

## Mkufunzi NCT Dk. Divecha: Mhudumu hoteli silaha kuu milango 5 ya fahamu

**Inatoka Uk.11**

Anasema alipomaliza 'Project ya Masters' yake kwenye mgahawa, alibahatika kumuandalia chakula Rais mstaafu wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, huku akimsifia.

"Kipindi hicho nakumbuka, Twiga, hoteli ya Kilimanjaro walifunga biashara. Watu wakubwa wote mawaziri walikuja kula kwangu. Mfano ukipewa aina ya visu kama 20, mhitimu upo 'field' (mafunzo vitendo) unajua namna ya kutumia. Hiyo inaweza kuwa mtihani wako wa kwanza, namna unavyoshika kila aina ya kisu ndiyo alama zako, zinazingatia uliyofundishwa," anasema.

### CHANGAMOTO

Dk. Divecha anasema kazi ya mapishi ina changamoto za ajira wakati mwingine na kawaida mwenye shahada ya juu hukosa kazi.

"Nina Phd ya Food ya Spices of The World. Lakini sababu ni viungo tu, unakuta hupati kazi. Ila nina kitu cha ziada. Ukarimu ni kitu cha kipekee," anasema.

Kuhusu vikwazo vya ajira pia anataja vingi vinakuwa vigezo vinavyoendana na fani hiyo, akisema mwonekano mzuri, lugha, maadili na ukarimu hutazamwa zaidi.

"Kama huna mbinu au hujui lugha mbalimbali, utasema kuna ubaguzi kwenye ajira hasa hotelini.

"Unatakiwa ujue angalau lugha tatu, zikiwamo Kifaransa, Kiingereza, hii itakufanya uwe mshindani. Sasa utakuta mhudumu hajui matamshi, hajui kusalimia vizuri, hana ukarimu wa kupokea mteja, utapataje kazi? Utaishia kusema unabaguliwa, unapokwenda kufanya 'field' (mafunzo kwa vitendo) uwe una vigezo vya ziada ili pale ulipo wasikuachilie," anasema Dk. Divecha.

Anasema zipo fursa za kuajiriwa hasa kwenye ofisi idara za mapokezi, huduma hiyo ikipata ambaye ana vigezo, mteja atarudi tena kesho.

"Ofisi nyingi tu hazina mapokezi. Hiyo ni fursa kwenu wahitimu . Ofisi lazima iwe na eneo la mapokezi. Tofauti na sasa kwenye mapokezi hukutani na huduma yenye ukarimu ili kesho urudi," anasema Divecha.

Pia hajasahau hali ya kuwa nadhifu muda wote, wenye tabasamu, na kumzingatia mteja 'kumteka' hata biashara inakua.



## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Jamani hizi kadi sasa zitatuachia magonjwa!




JUZI kati hapa niko njiani na ngalangala langu hili lenye mwendokasi wa '20 kks' zamani nikiliita gari, nikamwona dogo nadhani anasoma chekechea au shule ya vidudu kama tulivyokuwa tunaziita enzi hizo.

Dogo nikamwona kabisa ameelemewa na begi la mgongoni, lililosheheni kana kwamba ni wale mabibi enzi zetu wakienda kusenya kuni na kuzibeba mgongoni mithili ya gamba la kobe walahi.

Nikaingiwa na huruma, nikakanyaga breki lakini ngalangala likaenda kusimama kama mita 50 hivi kutoka alikokuwa dogo. Hata hivyo, akanifikia na nikamwita nikamuuliza hali akajibu "thalama thikamoo!"

Nikamwitikia na kumuuliza anakokwenda akanijibu tena kwa heshima tu: 'shule!' Nikamuuliza shule gani akanijibu, 'Dei thkuu!' Nikamwambia panda nikupeleke. Unajua tena vitoto kwa magari, haraka akaparamia, lakini begi likamzidi uzito.

Nikashuka na kumvua begi, ambalo hata nami nikahisi uzito mkononi, nikakaingiza ndani nikakapeleka shule. Nikakashusha na kukavalisha tena begi. Nikawakumbuka wale kina 'Adamoo' wa Uwanja wa Mkapa siku za sikukuu.

Nikakumbuka jinsi wataalamu wa afya wanavyohimiza karibu kila siku kupitia vyombo vya habari kuhusu mabegi mazito kwa watoto. Kwamba yanawaumiza migongo na huenda yakawaathiri uti wa mgongo baadaye.

Nikakihurumia sana kile kibwana mdogo na nikafikiria wanetu wote nchini wanaosoma shule za aina hii za



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

kubebeshana mabegi yamejaa makauntabuku yasiyo na umuhimu wowote badala ya kuwa na madaftari ya kawaida yaliyoandikwa 'Exercise Book', mbona yapo tu!

Hivi kwanini basi wenye shule zao hizo, wasiwe na mbinu za kujenga vijikabati -'lockers', kwa ajili ya kuhifadhi vitabu na madaftari hayo badala ya kuwabebesha watoto?

Au kama si hivyo, kwani walimu hawajui kuwa leo tuna masomo haya basi vitabu vya masomo yaliyo kwenye ratiba ndivyo vibebwe? Tena kwa mifuko ya mikononi, hata ya Rambo?

Kwa kweli Adolf Mkenda na Inno Bashungwa, mawaziri wetu jaribuni kulitafakari hili, kabla hamjampa msala wa kutibu Ummy Mwalimu, wenye shule zao hizi wanafanya vitoto vyetu vidumae na kuwa vibaunsa kabla ya umri wao jamani.

Pengine ndiyo sababu watu wanajiuliza, hivi kwanini siku hizi tunazaa vijeba tu na kutoa mfano hata kwa wachezaji wetu wa soka, siku hizi mbona hatuna watu kama kina Adam Sabu, Mohammed Tall, Peter Tino, Kitwana Manara na kina Sembuli?

Siku hizi eti tuna kina... eti ndio majayanti wetu katika soka. Huku kuelemewa kwa mizigo hivi sasa kumehamia hata kwetu watu wazima katika suala la vitambulisho, ambapo hivi sasa mtu anakuwa na kipochi kimefura utadhani kuna mabulungutu ya noti kumbe ni vitambulisho.

Fikiria kwenye pochi una NIDA, una kadi za benki si moja, kama u dereva una leseni, una kitambulisho cha kazini, hujakaa sawa una cha mpiga kura, kama ni chinga una kitambulisho cha uchinga, una cha Yanga au Simba, bado cha CCM au ACT-Wazalendo, wewe tu huyo, pochi moja.

Hivi kweli si kuumizana huko? Hilo pochi unalisondeka mfuko wa nyuma wa jinzi lako, hapo lazima ukikaa ukae upande upande, wataalamu wa tiba wanasema unaumiza nyonga na ukiendelea ulemavu unakujongea.

Sasa tunafanyaje waungwana? Hivi hakuna ujanja ambao unaweza kufanywa na Serikali sikivu kama hii, kwamba watu wawe na kitambulisho kimoja kitakachokuwa na mambo yote hayo, ya kazini, ya chamani, ya umachingani, ya vikoba, ya uchaguzi na ya chanjo ya Uviko nakadhalika, ili kuepukana na mizigo mifukoni.

Utakuta mtu kavimbisha mfuko wa nyuma ukidhani pengine ana fedha na kumhatarishia maisha yake na vibaka, kumbe ni kadi, kadi, kadi; vitambulisho, vitambulisho, vitambulisho!

Jamani, tuwe na kiasi basi, ili kadi moja ichukue yote. Vinginevyo wazee wazima hatutotofautiana na vichekechea vya mabegi. Alamsiki

## NUSU SIMBA DUNIANI WAPO NCHINI...

# Serikali yaja na mikakati kutanua utalii, utafiti aina yake ukiendelea

- Waziri Ndumbaro ajivuna rekodi watalii imevunjwa

**Na Maulid Mmbaga**

SEKTA ya Maliasili na Utalii nchini imekuwa iking'aaa na inaendelea hivyo. Ni miongoni mwa sekta muhimu na zinazopewa kipaumbele karibu kila nchi duniani kutokana na umuhimu wake katika kuchangia ukuaji uchumi kitaifa.

Tanzania nayo si kisiwa katika eneo hilo. Imewekeza nguvu kubwa katika sekta hiyo, huku kikikadiriwa zaidi ya asilimia 60 ya mauzo ya huduma hutokana na utalii, ikiwa ni miongoni mwa nchi duniani zenye vivutio vingi vya kitalii kama Mlima Kilimanjaro, Hifadhi za Serengeti, Ngorongoro na Mwalimu Nyerere.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro hivi karibuni ameshirki Mkutano wa 50 wa Mwaka wa Uwindaji wa Kitalii, nchini Marekani uliojadili ukuzaji wa sekta hiyo.



Namna ilivyo ustawi wa simba hifadhini na ongezeko la watalii nchini.**PICHA: MTANDAO.**

### KULIKONI SIMBA WENGI?

Katika mkutano huo, Rais wa Jumuiya ya Uwindaji ya Kimataifa, (SCI), Sven Lindqueast, anaitaja Tanzania kuwa nchi yenye nusu ya simba wote duniani, hivyo akaipongeza nchi kwa hatua za utunzaji mazingira na hifadhi, hali inayosaidia kuwapo wanyama hao wengi.

Dk. Ndumbaro anachangia hoja, ni zao linalotokana na juhudi za kiserikali katika kuboresha hifadhi zake, huku ikiwa imeruhusu uwindaji wa kitalii.

Anataja mfano, ni kuimarika shughuli za uhifadhi hususani kwa wanyamapori walao nyasi, wengi huwa ni mlo wa simba, hatima ya yote ni kuongezeka idadi ya wanyama hao, hali inayowapa simba uhakika wa mlo.

Waziri anafafanua, simba hula wanyamapori wanaotumia nyasi kama chakula, huku mlo huo wa simba ukiongezeka maradufu, kutokana na kuwapo nyasi za kutosha, ikiwa ni zao la usimamizi bora wa maeneo ya hifadhi.

Mchango mwingine kwa mujibu wa waziri, ni hatua za kiserikali kubadili mamlaka na utumishi unaosimamia hifadhi kutoka kiraia hadi kijeshi, nako kuna mchango mkubwa katika ongezeko la idadi ya simba kitaifa.

Eneo lingine analotaja waziri ni serikali kuitengea bajeti ya kutosha Wizara ya Maliasili na Utalii, inayotumika katika kuendesha operesheni za kukabiliana na ujangili, mazao yake yakionekana kwa ujangili kukomeshwa kwa zaidi ya asilimia 90, akisisitiza ifikapo 2025, ambayo ni miaka mitatu ijayo kunatarajiwa kumalizika kabisa tatizo la ujangili.

> “Fedha hizo zingeweza kutumika sehemu nyingine, ila Rais akaona aziingize huku ili ziweze kusaidia kuleta maendeleo katika sekta hii. Hivyo zitumike vizuri ili tufikie malengo

Katika orodha yake Dk, Ndumbaro anataja utolewaji wa elimu kwa jamii, akifafanua kwa sasa umma wa Watanzania unatambua umuhimu wa wanyamapori na wamekuwa wakitoa ushirikiano kwa serikali, kwa kutoa taarifa zinazohusu ujangili pindi unapotokea.

Anasema nchi imejiwekea utaratibu kuhakikisha wananchi wote wanaoishi katika maeneo ya hifadhi, wananufaika kwa kusogezewa huduma za kijamii, hata wanaona faida za kuwapo wanyamapori.

Dk. Ndumbaro ambaye kitaaluma ni mwanasheria, anasema sheria kali ya kutokuruhusu shughuli za kibinadamu hifadhini, imesaidia kufanya hifadhi zibaki katika uasilia wake, ikiwa na mchango wa moja kwa moja wa kuongezeka simba, pia wanyamapori wengine.

“Licha ya Tanzania kuwa na vitalu vya uwindaji wa kitalii zaidi ya 100, lakini imekuwa ikiendesha uwindaji huo kwa kuzingatia matumizi endelevu na ndiyo maana imezidi kuongoza duniani kwa kuwa na simba wengi,” anabainisha Dk. Ndumbaro.

### FAIDA UWINDAJI

Dk. Ndumbaro pia anapinga madai ya baadhi ya nchi zinazopinga Uwindaji wa Kitalii, kwa mtazamo ni utalii unaozipunguzia idadi ya wanyamapori.

Waziri anatetea uwindaji wa kitalii kuwa ni muhimu, kwa sababu unasaidia kupunguza ziada ya wanyamapori wanaotakiwa, wanaoweza kuwa na athari kwa binadamu jirani na wanakoishi wanyama hao.

Anasema kwa sasa Tanzania inakabiliwa na athari za kibinadamu kutokana na ongezeko la wanyamapori kama tembo pamoja na mamba.

Upande wa mikakati iliyopo, anataja serikali inajipanga kuhakikisha sekta hiyo inaendelea ikiwamo katika utoaji elimu sahihi ya kijamii, ili kuongezea umma ufahamu kwenye umuhimu wa utalii, pia kutafiti idadi ya watalii na mchango wa sekta hiyo kimaendeleo.

Waziri anasema dira iliyoko katika utafiti huo wa kitalii, sehemu ya matarajio ni kwamba itaiwezesha kuibua fursa za ajira kwa wazawa 700, watakaposhiriki kuinua utalii kitaifa.

Ni utafiti unaoratibiwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Waziri akisema utasaidia kujua sera, sheria, kanuni na miongozo inayotekeleza dira ya maendeleo ya miaka mitano, inayoonyesha jamii ilikotoka, iliko na inakoelekea, ikiwa ni namna ya kupanua wigo wa upokeaji watalii wa ndani na nje.

Waziri anataja dira ya kiserikali, ni kwamba mwaka 2021 watalii wa ndani waliongezeka hadi kufikia 700,000 na nje 900,000 akisifu imevunja rekodi zilizoko.

Hapo anafafanua, matarajio ni ifikapo mwaka 2025, mapato yanayotokana na sekta utalii yafikie Sh. bilioni sita na watalii wafikie milioni 25, akisisitiza angalizo fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji utafiti, zitumike kwa nidhamu.

“Fedha hizo zingeweza kutumika sehemu nyingine, ila Rais akaona aziingize huku ili ziweze kusaidia kuleta maendeleo katika sekta ya utalii nchini,” anasema Prof. Batinoluho... 

### MAELFU KAYA KUFIKIWA

Mshauri elekezi wa mradi kutoka OUT, Prof. Ladislaus Batinoluho, anasema ni utafiti unaotarajia kuzifikia zaidi ya kaya 33,800 zitakazotumiwa kukusanya taarifa za kupima ukubwa na mwenendo wa utalii nchini.

Anauelezea utafiti utasaidia kukadiria idadi ya watalii wa ndani na nje, pia katika utekelezaji wa ukusanyaji taarifa hizo, watawapatia mafunzo zaidi wataalamu 31 watakaowasaidia kukamilishaji suala hilo.

“Zaidi ya wakusanya taarifa 676 watatumika na utafiti huu utaendeshwa kwa muda wa miezi minne na takwimu zitakazotokana na tafiti hii, zitasaidia kuonyesha mwelekeo na kutoa ushauri mbalimbali utakaochochea maendeleo katika sekta ya utalii nchini,” anasema Prof. Batinoluho, anayepatikana katika Idara ya Utalii na Ukarimu.



## HABARI DODOMA

# Jiji lapewa maelekezo upandaji miti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Godwin Mollel, amelitaka Jiji la Dodoma kuwasimamia wananchi kupanda miti kama inavyofanyika kwenye usimamizi wa rangi za mabati zinazotambulisha mitaa.

Aidha, amesema uwapo wa mazingira safi kunaipunguzia serikali bajeti ya dawa.

Mollel aliyasema hayo alipoongoza zoezi la usafi wa mazingira kwenye soko la Chang'ombe na kutoa elimu ya utenganishaji wa taka, mifuko na vifungashio vya plastiki ikiwa ni sehemu ya Wiki ya Uzinduzi wa Sera ya Mazingira ya Mwaka 2021.

"Moja ya sifa mtu kuja nje kwako akute mazingira safi yenye miti ya kuvutia, sasa nyie Dodoma mmetupangia rangi za mabati, lakini hamjatupangia tuoteshaje miti, mmekomalia rangi za mabati kuliko uoteshaji miti, sasa jinsi mnavyosimamia watu wajenge nyumba zenye rangi gani tunaomba msimamie kila mtu aoteshe miti angalau 20 kwa mwaka huu," alisema.

Alihimiza wazazi kuwapatia watoto wao miti ya kuotesha maeneo ya shule ili atunze.

Hata hivyo, alisema maambukizi ya magonjwa mbalimbali ya mlipuko yanatokana na uharibifu wa mazingira.

"Gharama ya kusafisha mazingira ni kidogo kuliko gharama ya wewe kwenda hospitali kujitibu magonjwa yanayotokana na mazingira chafu," alisema.

Alisema pia kufanya usafi wa mazingira kunaongeza umri wa kuishi kwa kuwa watu wengi wanafariki kutokana na mazingira kuwa chafu.

"Watu wengi wanafariki na wengine kupunguza umri wa kuishi kutokana na magonjwa ambayo kama mazingira yakisafishwa hayatakupata," alisema.

Aliongeza: "Kidude cha soda kile kikiingia eneo ambalo kuna maji kina uwezo wa kuzalisha mbu 400, je, leo hapa kumekuwa na vidumu vingapi?Tumekuja kusafisha mazingira ili tusife."

Pamoja na hayo, alihimiza wananchi kuchanja chanjo ya UVIKO-19 ili kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo.

"Ujanja ni kuchanja, mjitokeze kuchanja serikali ilichelewa kutoa chanjo tulikuwa tunajiridhisha na sasa tumejiridhisha ni salama ndio maana hata Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa wa kwanza kuchanja," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mary Maganga alisema usafi huo ni mwendelezo wa shughuli ya wiki ya uzinduzi wa sera hiyo itakayozinduliwa kesho na Makamu wa Rais, Dk.Philip Mpango jijini hapo.

"Tumepanda miti maeneo mbalimbali Medeli, Iyumbu tukishirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) na Jiji la Dodoma kufanya usafi kwenye barabara na soko," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Mazingira wa Jiji hilo, Ally Mfinanga, alisema kuna umuhimu wananchi wakatenganisha taka ikiwamo za plastiki ili wananchi wajasiriamali wa taka hizo wazichukue na kuuza viwandani.

"Pia mabaki ya chakula yanasaidia kulisha mifugo, sisi tunasisitiza watu watenganishe taka kwa kuwa inasaidia halmashauri kupunguza gharama kubwa za kudhibiti taka ngumu ambapo asilimia 70 ya fedha hutumika kusafirisha taka," alisema.

# Jukwaa lashtukia miradi ya kilimo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JUKWAA la Wanawake Wakulima Wadogo Tanzania (JUWAWATA), limebaini zaidi ya miradi 61 ya kilimo kwenye mikoa mbalimbali ikiwamo Singida na Dodoma imetelekezwa na mingine haijafanyiwa ukarabati hali inayosababisha wakulima kukosa f ursa ya kujikwamua kiuchumi.

Rais wa Jukwaa hilo, Amina Senge, aliyasema hayo kwenye mkutano na wakurugenzi wa Wizara ya Kilimo, ulioitishwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Action Aid Tanzania kwa ajili ya kufanya tathmini ya miradi iliyokufa na ambayo haifanyi kazi.

Senge alisema miradi hiyo ilikuwa mkombozi mkubwa kwa wanawake, lakini haifanyi kazi na mingi imebadilishwa matumizi na kuiomba serikali kuifufua miradi hiyo mikubwa ya kilimo ili kuleta tija kwa wakulima.

Alitaja baadhi ya miradi hiyo ni ekari 560 za mradi wa umwagiliaji Kata ya Itilima ambao uligharimu Sh. milioni 302.13 mwaka 2005, lakini ulifanya kazi msimu mmoja tu.

"Mingine ni mradi wa umwagiliaji wa bustani uliogharimu Sh. milioni 298 katika kijiji cha Nyenze, lakini kwa miaka tisa haufanyi kazi huku majengo ya miradi ya kilimo Wilaya ya Chamwino mingi yamegeuzwa ofisi za watendaji," alisema.

Aliongeza "Majengo ya benki ya mazao, yamekuwa kumbi za starehe, viwanda vinajengwa, lakini TBS hawatoi vibali na baadhi ya vituo vimekuwa maghara ya kuhifadhia vifaa vya TASAF, tunaomba wizara iangalie hatima ya wakulima."

Alipendekeza Wizara ya Kilimo kuangalia uwezekano wa kuifufua baadhi ya miradi hiyo kwa awamu ili kuwarudishia matumaini kwa wakulima.

"Kuna miradi iliyokwama ni mingi, lakini tumeichukua kwa uchache kama mfano maana sehemu kubwa ya miradi imesahaulika na serikali haionyeshi namna gani inaijali miradi hiyo," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Bajeti na Mipango wa Wizara ya Kilimo, Timotheo Semuguruka, alisema serikali ipo mbioni kuifufua miradi hiyo ili kuwa na tija kwa wakulima.

"Tunapoelekea kwenye bajeti, baadhi ya miradi itaingizwa kwenye bajeti ili waanze kufufuliwa kwa kuwa inatia aibu mingine inatokana na fedha za wafadhili na wadau," alisema.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama (kulia), akipokea nakala ya Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu 2017-2022, kwa ajili ya rejea yake kutoka kwa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Neema Mwakalyelye, alipofanya ziara ya kikazi katika ofisi za TAKUKURU, jijini Dodoma juzi, yenye lengo la kujitambulisha na kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa taasisi hiyo. **PICHA: UTUMISHI**

# Ataka kuletwa mabadiliko chanya ukatili wa kijinsia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, ametaka utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) kuleta mabadiliko chanja kwa jamii ili kuondokana na vitendo hivyo.

Dk. Chaula alitoa kauli hiyo jijini hapo alipokuwa akifungua kikao cha kamati tendaji inayojumuisha idara na wizara zinazotekeleza mpango huo.

Alisema ni vyema kila mmoja kuwajibika ipasavyo kutekeleza mpango huo na matokeo yawe ya takwimu zitakazotumika kupanga namna ya kutatua kero zinazobainika.

Hata hivyo, alisema lazima kuwe na vigezo vya kuondoa matatizo ya ukatili yaliyoko ili matokeo yaonekane kuanzia ngazi ya vijiji na mitaa.

"Utendaji wetu wa kazi uwe na matokeo, mpango huu wa miaka mitano

kila mmoja atekeleze wajibu wake na

kazi yoyote uliyopewa lazima iwe na matokeo kwa takwimu," alisema Dk. Chaula.

Aliongeza kuwa kama kamati ikitekeleza majukumu yake, vitendo vya ukatili vitapungua na havitatokea katika jamii.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi wa Majaribio wa kutokomeza ukatili wa kingono, Geoffrey Chambua, alisema mradi huo uliofanyika kwa miezi mitatu Wilaya ya Kinondoni ilionekana kuna umuhimu wa kuwa na vituo vya mkono kwa mkono vinavyowasaidia waathirika wa ukatili wa kingono kupata huduma muhimu kwa pamoja na kwa wakati.

Naye Naibu Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo (WILDAF), Cesilia Assey, alipongeza serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kwa karibu na kutoa wito kwa wadau wote kushirikiana kutokomeza tatizo la ukatili.

Aidha, alisema lengo ni kufikia hatua ya huduma kwa waathirika wa ukatili zinapatikana kwa urahisi na wananchi wanafikiwa kupata elimu kuhusu madhara ya ukatili katika jamii.



# Waathirika 170 dawa za kulevya waacha dawa na kukimbia kliniki

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya waraibu 170 wa dawa za kulevya kati ya 435 walioandikishwa kutumia dawa katika kliniki ya Methadone mkoani Mbeya, hawajulikani waliko baada ya kuachana na dawa hizo na kutokomea kusikojulikana.

Daktari bingwa wa magonjwa ya akili katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, mahali iliko kliniki ya Methadone inayohudumia waraibu wa dawa za kulevya, Dk. Beatrice Thadei, alisema hadi kufika mwisho wa Januari, mwaka huu, waraibu 435 waliandikishwa na kwamba 171 hawajulikani waliko.

Alisema kliniki ya Methadone Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilizinduliwa mwaka 2017 kwa lengo la kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi baada ya kubaini kuwa idadi kubwa ya waraibu ni waathirika wa Ukimwi.

Dk. Thadei alisema kliniki hiyo inatoa huduma mbalimbali za kuwasaidia waraibu wa dawa za kulevya zikiwamo kifua kikuu, magonjwa ya ngono na kuwaunganisha na familia zao kuwafanya waraibu waendelee kutumia dawa.

"Tangu kuanzishwa kwa kliniki hii, waraibu 53 waliachana na matumizi ya dawa za kulevya kwa kumaliza dawa huku wakiendelea kufuatiliwa kuhakikisha hawatumii tena dawa.

"Waraibu 171 hawajulikani waliko, hivyo wamejiondoa kwenye mradi. Tisa tuliwachukua kutoka kwenye vituo vingine, waraibu 13 walihamishiwa vituo vingine," alisema Dk. Thadei.

Aliongeza kuwa waraibu 17 kwa sasa katika kliniki hiyo, wanamaambukizi ya virusi vya Ukimwi na kwamba tangu kuanza kwa kliniki hiyo, waraibu 52 walioathirika na Ukimwi, kati yao wanane wakipoteza maisha na 12 hawapo kwenye kliniki kwa sasa.

Dk. Thadei alibainisha kuwa miongoni mwa vikwazo vinavyowakabili baada ya kuanzisha kliniki hiyo ni waraibu kusumbua kutumia dawa baada ya kupata nafuu, kuendelea kuvuta bangi au kunywa pombe.

Hata hivyo, wadau wa mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya mkoani Mbeya, wameliomba Jeshi la Polisi kutoa mafunzo kwa askari wake kuhusu masuala ya upunguzaji wa madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Walisema mafunzo hayo yatasaidia askari hao pindi wanapowakamata vijana wanaokinzana na sheria walio kwenye tiba ya maradhi hayo, wasikatishe dozi kwa kuwa kufanya hivyo wanarudisha nyuma vita dhidi ya dawa za kulevya na Ukimwi.

Ofisa Kinga kutoka Shirika la HJFMRI, Damali Lucas, alitoa ombi hilo wakati wa kuhitimisha mkutano wa siku mbili wa wadau mbalimbali wa dawa za kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya uliofanyika mkoani Mbeya.

Alisema mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwapa elimu watumishi wa vyombo vya ulinzi na wadau wengine kujifunza namna gani ya kuwahudumia warahibu wa dawa za kulevya ili kukabiliana na unyanyapaa.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Mbeya, Joseph Mwasote maarufu China (aliyevaa kofia nyekundu mbele), akiwa na wafuasi wa chama hicho katika ofisi za Kanda ya Nyasa, jijini Mbeya, kwa ajili ya kuunda kamati mbalimbali baada ya viongozi waliokuwapo kuvuliwa uongozi wiki iliyopita. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TAKUKURU yapokea taarifa 109 za rushwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAARIFA mpya 109 za tuhuma za rushwa na makosa mengine zimepokewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU) katika kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Desemba, 2021.

Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Abdaudi Mbura, alisema jana kuwa kati ya hizo, taarifa 69 zilihusu rushwa na 40 hazikuhusu rushwa.

Alibainisha kuwa madai 20 yaliripotiwa kwenye halmashauri mbalimbali, mahakama kesi 12, polisi kesi tano, afya kesi nane, sekta binafsi (wafanyabiashara) kesi 20 na ardhi kesi 12.

Mashirika ya umma kesi 12, vyama vya ushirika kesi nne, ujenzi kesi mbili, maliasili tano, elimu kesi saba na fedha kesi mbili.

"Kwa upande wa mashtaka katika kipindi hiki, tumefungua kesi mpya sita mahakamani kwa makosa mbalimbali na kufanya tuwe na kesi 25 zilizoendeshwa. Hata hivyo, kesi iliyoamuliwa ni moja tu na kati ya hizo TAKUKURU ilishinda kesi moja," alisema Mbura.

Katika hatua nyingine, TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, ilianzisha operesheni maalum ambayo ilipewa jina la Kata kwa Kata lengo likiwa ni kufuatilia ufanisi wa matumizi ya sheria na miongozo mbalimbali iliyotolewa kuhusu utekelezaji wa majukumu iliyotolewa kuhusu uongozi kwenye ngazi ya kata.

Katika operesheni hiyo, TAKUKURU ilibaini mianya ya rushwa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya viongozi wa kata pamoja na kubaini thamani ya fedha katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwenye kata ukilinganisha na hali halisi ya mradi unavyoonekana.

Aidha, TAKUKURU iliwafikia wananchi 2,913 kwa lengo la kujengewa uwezo juu ya madhara ya rushwa na kushiriki kikamilifu mapambano dhidi ya rushwa ambapo semina 11 ziliendeshwa pamoja na kuanzisha klabu za wapinga rushwa shule za msingi na sekondari.

# Waliofeli darasa la saba wapelekwa VETA

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya wanafunzi 3,000 waliofeli mtihani wa darasa la saba mwaka 2021 mkoani Mbeya, wamepelekwa kwenye Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) na vile vya maendeleo ya wananchi.

Lengo la wanafunzi hao kuwapeleka kwenye vyuo hivyo ni kupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa na kuwaepusha kujiunga na makundi hatarishi kama vile uvutaji bangi, watoto wa mitaani na mimba za utotoni.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema hayo juzi alipozungumza na Nipashe juu ya mikakati ya serikali kuwawezesha wanafunzi waliofeli mtihani wa darasa la saba.

"Kwa mwaka 2022, serikali ya mkoa wa Mbeya inawapeleka vyuo vya ufundi wanafunzi 3,170 waliofeli mtihani wa kuhitimu darasa la saba ili kuwaepusha watoto wadogo kuajiriwa mitaani, watoto hao watajifunza ujuzi wa aina mbalimbali ikiwamo ufundi umeme," alisema Homera.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Ernest Hinju, alisema kati ya wanafunzi 44,818 waliofanya mtihani wa darasa la saba, 5,314 hawakufaulu, hivyo kukosa nafasi ya kuendelea na masomo.

Alisema kati ya watahiniwa 44,818 waliofanya mtihani mwaka 2021, wanafunzi 39,504 walifaulu mtihani huo na kupangiwa shule.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, aliwataka wadau wa elimu hasa walimu kuongeza jitihada za kuwaelimisha wanafunzi ili kuhakikisha mkoa unazidi kufanya vizuri katika mitihani ya kitaifa.

"Nawaomba wadau wote wa elimu tusiridhike na matokeo ya mwaka huu bado tuna kazi kubwa ya kufanya ili kuhakikisha mkoa unaendelea kufanya vizuri na hatimaye kutimiza ndoto za watoto wetu na kuipa sifa njema Mbeya yetu," alisema.



# Taasisi ya Turky kuanzishwa kusaidia yatima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya Vigor inatarajia kuzindua mfuko wa kusaidia watoto yatima ambao utajulikana kwa jina la Salum Turky Foundation, ikiwa ni hatua ya kuendeleza malengo ya mfanyabiashara maarufu na aliyekuwa Mbunge wa Mpendae, Salum Hassan Turky, aliyefariki dunia mwaka 2020.

Akizungumza jana mjini Zanzibar na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Adallah Salum Turky, alisema mwazilishi wa Vigor, Salum Turky, wakati wa uhai wake, alikuwa na malengo ya kusaidia maskini na watoto yatima katika nyanja mbalimbali zikiwamo elimu, afya na ajira.

Turky alisema mfuko huo utazinduliwa mwezi ujao na utasaidia yatima na watu maskini ili kupata huduma muhimu za kijamii na kutojihisi wanyonge kutokana na hali waliyo nayo.

Alisema lengo la Vigor ni kusaidia jamii ikiwamo kuwapatia ajira wananchi na kushirikiana na serikali katika kuimarisha nchi.

Pia alisema katika kumuenzi mwanzilishi wa kampuni hiyo, wanatarajia kuzindua kitabu maalum ambacho kinaelezea maisha yake na changamoto alizopitia tokea alivyoanza kufanya biashara mwaka 1988 kwa kuanza na biashara ya kuuza mifuko na hatimaye kuwa mfanyabiashara mkubwa.

"Kitabu hicho kitakuwa kinaitwa Safari ya Mr White, ambalo ni jina maarufu alilokuwa akitumia mwazilishi wa kampuni hii ya Vigor," alisema.

Alisema mwazilishi huyo alipitia changamoto nyingi bila kukata tamaa ambapo alitokea katika familia maskini lakini kutokana na shida alizopitia, alisonga mbele na hatimaye kuwa mfanyabiashara mkubwa hadi mauti yalipomfika.

Wakizungumzia azma ya kuanzishwa mfuko huo, baadhi ya wananchi walisema utasaidia kupunguza changamoto za watoto yatima na maskini nchini.

"Kwa sasa utagundua kwamba kila taasisi inajitokeza kulea yatima lakini hawana msaada wowote, hivyo mfuko huo unaweza kupunguza changamoto hasa upatikanaji wa rasilimali fedha," alisema Mussa Said, mkazi wa Fuoni.

Fatma Massoud, mkazi wa kijiji cha Nungwi, ambaye analea watoto yatima baada ya baba yao kufariki dunia katika ajali ya meli ya Mv Spice Islander mwaka 2010, alisema mfuko huo unaweza kusaidia kuwaweka watoto yatima katika maisha sawa na watoto wengine hasa kupata haki ya elimu.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Vigor, Abdallah Turky (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, kuhusu uzinduzi wa Salum Turky Foundation kwa ajili ya kumuenzi aliyekuwa mfanyabiashara maarufu na Mbunge wa Jimbo la Mpendae, aliyefariki dunia mwaka 2020. Kulia ni Meneja wa kampuni hiyo, Haytham Turky. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Othman ajivunia uzoefu serikalini

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema uzoefu wa kufanya kazi na viongozi tofauti serikalini umemwezesha kujifunza mengi ya siasa na utendaji.

Othman aliyasema hayo katika mahojiano maalum na Radio Alnoor nyumbani kwake, Chukwani, akieleza maisha yake ya kisiasa kuelekea mwaka mmoja tangu kuteuliwa kushika wadhifa huo.

Alisema katika maisha yake yote ya utumishi wa serikali amefanya kazi na wanasiasa mbalimbali kwa zaidi ya miaka 25 jambo lililomsaidia kupata uzoefu na kujifunza masuala mengi kutoka kwao.

Pia alisema jambo hilo limemsaidia kufahamu changamoto na namna wanasiasa wanavyofanya kazi na kwamba jambo hilo limempa unafuu wa kufahamu kazi na mazingira ya shughuli za kisiasa.

Alisema ugumu na changamoto za kisiasa ya vyama vingi katika kipindi cha miaka ya 1990 na kwa mazingira ya Zanzibar, haikuwa rahisi kwa mtu wa kawaida kukubali kubeba dhamana kubwa za kusimamia nchi.

Akizungumzia suala la kisiasa na marehemu Maalim Seif Sharif Hamad, Othman alisema kiongozi huyo alitoa mchango mkubwa na muhimu katika kusimamia na kurejesha amani, kuondoa chuki na ugomvi kiasi kwamba wanzibari wakuwa kitu kimoja.

Alisema kwamba shughuli za uendeshaji siasa nchini Tanzania hivi sasa zinatia moyo kutokana na kuwapo matumaini kwa juhudi zinazofanywa za kurekebisha masuala mbalimbali ya kisiasa kupitia kikosi kazi kilichoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Pia alisema siasa za Tanzania hivi sasa zinahitaji kutengenezewa mazingira ya kuwapo mageuzi makubwa kupitia mijadala ya kitaifa kuhusu masuala yanayohusu nchi na uendeshaji wake jambo litakalosaidia kuufanya mfumo wa siasa za nchi kuwa bora zaidi.

Alisema yako masuala mengi ya msingi ambayo uelewa wa wananchi ni mdogo na kwamba wanahitaji kuyaelewa, hivyo kuwapo kwa mijadala ya namna hiyo kutasaidia kuwajengea uwezo mkubwa wananchi kufanya uamuzi sahihi wa masuala yanayohusu nchi.

# KMKM yaokoa mabaharia, mafuta katika jahazi lililozama baharini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIKOSI Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimeokoa mabaharia wanane kati ya tisa na madumu 1,400 ya mafuta ya kupikia baada ya jahazi lililokuwa likisafirisha bidhaa hiyo kuzama katika eneo la Bumbwini, mkoa wa Kaskazini Unguja.

Jahazi hilo liliondoka katika Bandari ya Malindi Februari 5, mwaka huu, kwenda Pangani, Tanga lakini likiwa njiani lilipata hitilafu na kuzama likiwa na mabaharia tisa ambao wote waliokolewa wakiwa hai.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa KMKM, Mkuu wa Doria wa kikosi hicho, Hussein Ali Makame, alisema baada ya kuokoa mafuta hayo waliyakabidhi kwa mmiliki wa jahazi hilo.

Makame alisema baada ya kupata taarifa ya kuzama kwa jahazi hilo, kikosi hicho kilifika kuwaokoa mabaharia tisa waliokuwamo ndani pamoja na mizigo iliyokuwamo.

Alisema baada ya kufika katika eneo la tukio, baadhi ya wavuvi walikuwa wameanza kuyapora madumu hayo na mengine waliyakuta pembezoni mwa bahari katika maeneo tofauti ya bahari eneo la Bumbwini.

Naye Mkuu wa Idara ya Sheria KMKM, Ismail Kaaya, alisema mmiliki wa mafuta hayo, amekabidhiwa mzigo wake baada ya kukamilisha nyaraka zote zikiwamo zinazoonyesha malipo ya ununuzi wa mzigo, nyaraka za ruhusa ya kusafirisha mzigo pamoja na nyaraka zingine ambazo zinaonyesha chombo kilichopakia mzigo kiliondokea katika bandari halali ya Malindi.

Mkuu huyo pia alisema kwa mujibu wa sheria za ukamataji za KMKM, watu hao walikuwa wakisafirisha mzigo kihalali na haukuwa na shaka yoyote.

"Mkuu wetu wa KMKM Komodoo Azana Msingiri aliridhia mmiliki huyo kupatiwa mzigo wake baada ya kuridhika na vielelezo vya tajiri huyo," alisema.

Aliwataka wafanyabiashara kuondoka katika bandari halali zilizoruhusiwa na kuiga mfano wa mmiliki huyo kwa sababu linapotokea tatizo, inakuwa rahisi kusaidiwa na kupatiwa mzigo wake bila tatizo lolote.

Mohammed Masoud, mdhamini wa kampuni ya First Delivery kwa niaba ya mmiliki wa kampuni hiyo, ameishukuru KMKM kwa msaada na ushirikiano mkubwa waliowapa kuanzia siku ya tukio la kuzama mabaharia wao ambao walifika kuwaokoa, lakini kwa kuchukua jukumu la kuwahifadhia mafuta yao kwa uaminifu mkubwa.

Mzigo huo uliokolewa ni wa madumu 1,400 na kila dumu lina ujazo wa lita 20. Gharama ya mzigo huo inakadiriwa kuwa zaidi ya Sh. milioni 100.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

**KINGAS KINGS COMPANY LIMTED** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI yenye namba za usajili **T478 BQN**
Chassis namba: **LE8PCJL30A2001682**
Injini namba : **FH156FM10C07061**
Kadi Namba **: 358377**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi
taarifa ya polisi RB namba **MKB/TR/RB/2230/2021**

116700502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 109 YA mwaka 2021**

**BAINA YA TUMSIFU APOLO BESSA NTANDU**
**(Suing as the Administrator of the Estate**
**OF the late APOLO BESSA NTANDU) ……………………MDAI**

**DHIDI YA**

**WILSON S. LUPIA……………………………………MDAIWA 1**
**JOYCE M. ANDREA……………………………………MDAIWA 2**
**AMINA B. TINA…………………………………MDAIWA 3**

**KWA: AMINA B. TINA**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 12.04.2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANAGALIZO: kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 10 ya mwezi Februari,2022.

116700202

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 17/2021**

**In the matter of the Estate of the late ELIELI PAUL MWALUKO**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JOHN ZEFANIA CHILIGATI**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 of PROBATE RULES GN 369 of 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 28/02/2022

**Date at Dodoma this 03rd Day of January 2022.**

RESIDENT MAGISTRATE

116700102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 148 YA mwaka 2020**
**BAINA YA**
**SHOMARI HUSSEIN MAGONGA……………………………………MDAI**
**DHIDI YA**
**MWITA MWITA……………………………………MDAIWA**

**KWA: MWITA MWITA**
**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 05.04.2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANAGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 09 ya mwezi Februari,2022.

116700002

---

## CHANGE OF NAME BY DEEP POLL
**Registration of Documents Act**
**(Cap.117)**

BY THIS DEED. I **PROSISTA GERALD MTEY** of Rombo District, Kilimanjaro Region, formerly known as **PROSISTA SIGISFRID TARIMO SWAI**. DO HEREBY absolutely renounce, relinquish and abandon the use of my former names and in lieu thereof do assume as from the date hereof the name **PROSISTA GERALD MTEY.**
**AND IN PURSUANCE** of such change of name as aforesaid, I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deeds, instruments, certificates and upon all occasions whatsoever use and sign the new name of **PROSISTA GERALD MTEY** as my name in lieu of the said former name of **PROSISTA SIGSFRID TARIMO SWAI** renounced as aforesaid.
**AND I HEREBY AUTHORISE** and request all persons to designate and address me in the new name of **PROSISTA GERALD MTEY**
**IN WITNESS WHEREOF** I hereunto set my signature in the manner and on the day and year hereinafter appearing.
**SIGNED and DELIVERED** by the said **PROSISTA GERALD** MTEY in my presence this 12 day of May 2021…………………………… DEPONENT

BEFORE ME:
COMMISSIONER FOR OATHS

1167003O2

---

## ENEO LA BIASHARA LINAPANGISHWA KWA MUDA MREFU [MIAKA 15-20] AU KUUZWA.

ENEO LA BIASHARA LENYE UKUBWA ZAIDI YA SQUARE METER 5,800 AMBALO LIPO MAENEO YA BARABARA YA MANDELA KARIBU KABISA NA UWANJA WA TAIFA DAR ES SALAAM.

216700601

**[Mwenye ofa kubwa atapewa kipaumbele]**
**MAWASILIANO**
**0762215470 MR MATHIAS**
**0682243694 MR. VALENCE**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa Kwa***
***Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

**HABARI KIMATAIFA**

## Waziri Mkuu Libya anusurika kuuawa

**Tripoli,** LIBYA

WAZIRI Mkuu Libya, Abdulhamid al-Dbeibah amenusurika katika jaribio la mauaji lililofanywa na watu wasiojulikana.

Gari lake lilishambuliwa kwa risasi lilipokuwa likiendeshwa katika mji mkuu, Tripoli, mapema Alhamisi.

Watu wenye silaha walikimbia eneo la tukio.

Pande zinazozozana zimekuwa zikigombea udhibiti wa Libya na bunge lenye makao yake Mashariki mwa nchi hiyo litapiga kura baadaye Alhamisi kumchagua Waziri Mkuu, atakayechukua nafasi ya serikali ya umoja wa kitaifa.

Dbeibah alisema, atapuuza matokeo ya kura hiyo.

Uchaguzi wa kuichagua serikali mpya, uliahirishwa Desemba, mwaka jana, hakuna kura inayotarajiwa kupigwa mwaka huu.

**BBC**

## China yaitaka Marekani iondoe vikwazo kibiashara

**Washington,** MAREKANI

CHINA imeyapinga madai kwamba ilishindwa kuyasimamia makubaliano ya kibiashara na Marekani ya mwaka 2020 na badala yake, imeitaka Washington kuiondolea mara moja kodi na vikwazo ilivyoviweka.

Matamshi hayo yanatolewa wakati Jumanne, wiki hii, Marekani ikichapisha takwimu zilizoonyesha nakisi ya biashara na China ikiongezeka kwa shilingi bilioni sita na kufikia jumla ya dola bilioni 34, mwezi Desemba mwaka jana.

Baada ya mzozo wa muda mrefu, mataifa hayo mawili yalifikia makubaliano yaliyoitwa awamu ya kwanza, Januari 2020, Beijing iliahidi kuongeza manunuzi ya bidhaa na huduma za Marekani kwa angalau dola bilioni 200 kwa mwaka 2020 na 2021.

Hata hivyo baada ya makubaliano hayo kulishuhudiwa mvutano wa kibiashara yaliyosababisha aliyekuwa Rais wa Marekani Donald Trump na Xi Jinping wa China, kuwekeana kodi za visasi za mabilioni ya dola.

Washington inalalamika kwamba, Beijing haisimamii ahadi zake kwenye makubaliano hayo huku takwimu zikionyesha wazi kuna upungufu huo.

**DW**

# Uganda yasema agizo la ICJ la kulipa fidia halikufikiwa kwa haki

**Kampala,** UGANDA

UGANDA imesema uamuzi wa Mahakama ya Kimataifa ya Haki ya kuamuru nchi hiyo kuilipa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), dola milioni 325 kama fidia, haukufikia kiwango cha haki kilichotarajiwa.

Katika taarifa yake, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kiryowa Kiwanuka, alisema nchi hiyo inapinga na inakataa kunyooshewa kidole cha lawama askari wa Uganda kwa makosa, licha ya mahakama kukiri kuwapo kwa makundi mengine yenye silaha nchini DRC.

Alitaja uamuzi wa mahakama kuwa ni kushindwa kuthamini masuala ya Afrika na kwamba hautoi mchango wowote katika juhudi za sasa za kutatua masuala ya usalama yanayoendelea huko.

Vikosi vya Uganda kwa sasa viko Mashariki mwa DRC, wakati huu kwa idhini ya Kinshasa kupigana dhidi ya waasi wa Islamic State, Allied Democratic Force (ADF).

Serikali ya Uganda, pia ni sehemu ya kufadhili ujenzi unaoendelea wa barabara ya kilomita 200 ili kuimarisha biashara kati ya nchi hizo mbili.

Mwaka 1999, DRC iliwasilisha kesi mbele ya ICJ dhidi ya Uganda kwa vitendo vya uvamizi wa silaha katika eneo lake kinyume na mikataba ya Umoja wa Mataifa (UN) na AU kati ya 1998 na 2003.

Wakati huo, Uganda haikuomba idhini ya serikali ya DRC, kuingia.

Katika kilele cha mzozo huo, zaidi ya nchi tisa za kiafrika ziliingizwa kwenye mapigano.

Kutokana na uamuzi wa mahakama siku ya Jumatano, wiki hii, Uganda sasa italazimika kulipa fidia hiyo kwa awamu ya dola milioni 65 kila tarehe 1 ya mwezi Septemba, kuanzia mwaka huu.

**BBC**




Gari la kijeshi ambalo limeonekana katika eneo la zamani la kivita tangu kutokea kwa vita baridi kati ya Urusi na Belarus. Umoja wa Kujihami wa Nchi za Magharibi (NATO), umedai Urusi imeanza 'chokochoko' jirani na mpaka wa Ukraine. **PICHA: AP**

# Mkuu MFDC aishutumu jumuiya ya ECOWAS

**Dakar,** SENEGAL

WAKATI wa mapigano yaliyotokea Januari 24, mwaka huu, yanayodaiwa kutekelezwa na waasi wa MFDC, wanajeshi wanne wa Senegal, waliuawa.

Kwa mujibu wa makao makuu ya jeshi huko Dakar, na wengine saba bado wanashikiliwa mateka na kundi la waasi eneo la Casamance, karibu na mpaka wa Gambia.

Katika eneo la makabiliano, shirika la habari la RFI limekutana na kiongozi wa waasi Salif Sadio, ambaye anawashutumu wanajeshi wa kikosi cha ECOWAS kuwa sababu ya makabiliano hayo.

Baada ya saa kadhaa msituni, hatimaye waandishi wa RFI waliwasili Bajagar, mji wa Casamance ulio karibu na mpaka wa Gambia, ambako Salif Sadio, kiongozi wa waasi wa MFDC na wapiganaji wake wameweka moja ya kambi zao. Akihojiwa na RFI, kiongozi wa waasi amerejea mapigano yaliyotokea Januari 24, mwaka huu.

"Kitu cha kusikitisha kilitokea. Wanajeshi wenye silaha kutoka eneo la Gambia walikuja kushambulia kambi zetu, wakiwa na silaha nzito. Wakati wa shambulio hili, tuliua wanajeshi wawili na tunawashikilia wengine saba, ambao tuliwakamata wakiwa na silaha mkononi.

"Wanajeshi hao, kila mmoja alisema ni sehemu ya wanajeshi wa ECOWAS, walioko nchini Gambia. Kwa malengo gani, kulinda serikali iliyoko madarakani, ndivyo walivyosema. Hata hivyo, nina wafungwa saba hapa mnaponiona. Mapigano yalitokea katika eneo la Casamance, walivuka mpaka kuja kunishambulia.

"Nilirudisha miili ya askari waliouawa kwa ECOWAS kwa sababu ECOWAS ilipotambua kuwa walikuwa wanajeshi wake, ilibidi tuwarudishie miili ya askari,"

"Sijui nitawarejesha kwa nani ikiwa sio ECOWAS," amejibu kiongozi wa waasi, wahusika hata hivyo! Kwa sababu ikiwa wajumbe wao watapendezwa kuja kuzungumza nami. Ikiwa masharti yatakamilika, wataachiliwa huru mara moja.

"Mnamo 2012, nilirudisha wafungwa wa Senegal - kutoka jeshi la Senegal, bila masharti! Kama kweli Senegal wamejitolea kujadili, kukaa chini kuzungumza kwa amani na MFDC kutatua tatizo la Casamance, tatizo liko wapi, wafungwa nitawarudisha kwao," alidai kiongozi huyo.

Salif Sadio alianzisha mazungumzo ya amani baada ya mapigano ya Januari 24, mwaka huu.

**RFI**

HABARI MICHEZO

# MAFUNZO YAMALIZA UBABE WA KMKM LIGI KUU ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KWA mara ya kwanza KMKM imekubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Mafunzo katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Gombani juzi visiwani hapo.

Hata hivyo mabaharia hao wa KMKM ambao wamecheza michezo 17 katika ligi hiyo ambayo inadhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), inaendelea kuongoza kwenye msimamo ikiwa na pointi 36.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema ameyapokea matokeo hayo na anaamini kupoteza kwa mchezo huo kwa sababu bahati haikuwa kwao kwa siku ya juzi.

**Msimu alisema hawezi kuwalaumu chochote wachezaji kutokana na kufungwa mchezo huo kwa sababu walicheza kwa kujituma katika dakika zote 90.**

"Niseme tu kwa ufupi kuwa bahati haikuwa yetu, wachezaji walijituma kuhakikisha wanaendeleza rekodi yao ya kutopoteza kwa kufungwa lakini ilishindikana, licha ya baadhi ya wachezaji kuwa na mapungufu, lakini walijituma kwa kiwango cha juu," alisema Msimu.

Kocha huyo aliongeza anaendelea kujipanga kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vyema katika michezo yao inayofuata na kujiimarisha kwenye mbio za ubingwa.

"Ninajua ligi ni ngumu, kila timu imefanya usajili na maandalizi mazuri kwa ajili ya kupata ushindi, tutaendelea kupambana na hatujakata tamaa kwa matokeo ya jana (juzi)," alisema kocha huyo. Alisema wanawataka mashabiki wao watulie na hawatarudia makosa katika mechi yao inayofuata ambayo watacheza dhidi ya Black Sailor.

"Tunajua bado tuna michezo mingi mbele yetu, kwa sasa tunajipanga kuikabili Black Sailor, tutashuka dimbani katika mechi hiyo kwa kufuta makosa tuliyoyafanya nyuma, tunajua kiu yetu ni kutetea tena ubingwa," aliongeza Ame.



Wanafunzi wa shule mbalimbali za sekondari Dar es Salaam wakichuana katika mpira wa kikapu kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Rashid, Mahlangu kurejeana Feb. 25

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Tonny Rashid, anatarajia kuzichapa na Bongani Mahlangu kutoka Afika Kusini katika pambano la kimataifa la marudiano litakalofanyika Februari 25, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Pambano hilo la kuwania mkanda wa ubingwa wa UBO na WBC litakuwa na uzito wa Super Bantama la raundi 10 na limepangwa kufanyika kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza jijini.

Tonny aliliambia gazeti hili jana amejiandaa vyema kuhakikisha anarejesha mkanda wake wa UBO na kushinda mkanda huo mwingine wa WBC.

"Nimejipanga ili kushinda pambano hili ambalo linasumbuliwa kwa hamu na mashabiki zangu pamoja na wadau wa ndondi hapa nchini, pia ninahitaji kurudisha furaha za Watanzania wote baada ya kushindwa kutetea mkanda wa UBO mwaka jana," alisema Tonny.

Aliongeza makosa yaliyojitokeza katika pambano la mwaka jana ameshayafanyia kazi kwa kushirikiana na kocha wake na tayari amempa 'silaha kali' za kuondoka na ushindi.

## Geita Gold FC yaiwinda Mbuni

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Geita Gold FC kimesema kiko tayari kuwakabili Mbuni FC katika mechi ya raundi ya 16 bora ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha.

Ofisa Habari wa Geita Gold, Hemed Kivuyo, alisema baada ya mapumziko ya siku moja, baada ya mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Polisi Tanzania na kushinda mabao 3-1, kikosi chao kiliianza tena mazoezi kwa ajili ya mechi hiyo ya mtoano.

"Baada ya mapumziko ya siku moja tulipocheza mechi ya Ligi Kuu, sasa tuko tayari kwa ajili ya mechi ya Kombe la FA, tunajua mechi zote ni ngumu, tunacheza dhidi ya Mbuni FC ambayo imeonyesha kukomaa siku za karibuni," Kivuyo alisema.

Geita Gold ilitinga katika hatua hiyo baada ya kuichapa Tunduru Korosho mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu, huku Mbuni FC ikiiondosha Lipuli FC kwa penalti 4-3 baada ya dakika 90 za kawaida kumalizika wakiwa suluhu.

# Pete wanaume kuchuana Morocco

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Netiboli Tanzania (CHANETA), kimesema Timu ya Taifa ya Wanaume ya mchezo huo inaendelea vyema na maandalizi kwa ajili ya kushiriki mashindano ya kuwania kombe la kimataifa yatakayofanyika kuanzia Machi 26, mwaka huu, nchini Morocco.

Mwenyekiti wa CHANETA, Devotha Marwa, alisema kwa sasa wachezaji wanafanya mazoezi ya pamoja na hapo baadaye wataandaa mashindano ambayo yatasaidia kupata nyota watakaounda kikosi cha taifa.

Marwa alisema kikosi cha timu hiyo kitaundwa kwa kuchanganya wachezaji wenye ubora wa juu kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

"Hivi karibuni tutaandaa mashindano ili tuangalie wachezaji ambao watafanya vizuri na kuwateua kwa ajili ya kwenda kushiriki mashindano hayo ya kimataifa," alisema Marwa.

Hata hivyo Marwa amewaomba wadau wa michezo kuisaidia CHANETA katika maandalizi ya kufanikisha safari hiyo ya kwenda Morocco.

"Nina imani timu tutakayoichagua itakwenda kufanya vizuri katika michuano hiyo, Tanzania tuna wachezaji wengi wazuri na wenye uzoefu," Marwa alisema.

## ZISIKUPITE

### HAALAND KUFANYA KWELI

KOCHA wa Borussia Dortmund, Marco Rose amesema mazungumzo ya "kweli" yanafanyika na mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 akiamua la kufanya kuhusu mustakabali wake. ***(Bild, via Mirror)***

### POCHETTINO AKARIBIA UNITED

WACHEZAJI kadhaa wa Manchester United wanataka klabu hiyo kuongeza juhudi za kumteua kocha wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino kama kocha ajaye ndani ya Old Trafford. ***(Express)***

### BABA DIAZI AFUNGUKA

BABA mzazi wa winga Colombia, Luis Diaz anadai kusita kwa Tottenham Hotspur kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kuliwaruhusu Liverpool kuwashinda na kumsajili mtoto wake. ***(Blu Radio,via Metro)***

### CHELSEA YAMBAKISHA RUDIGER

CHELSEA imempa mchezaji wa kimataifa wa Ujerumani, Antonio Rudiger mkataba mpya utakaomfanya kulipwa pauni 200,000 kwa wiki katika jitihada za kumbakisha beki huyo mwenye umri wa miaka 28 ambaye anabakia hapo Stamford Bridge. ***(Goal)***

### BISSOUMA SOKONI RASMI

KLABU ya Brighton inaweza kutarajia kufufua nia ya Aston Villa kumnunua kiungo wa kati wa Mali, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 25, msimu huu baada ya kukataa dau la pauni milioni 35 katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Athletic)***

### MARTIAL ALIITAKA SEVILLA

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 26, anasema Barcelona na Juventus walikuwa na nia ya kumsajili Januari, lakini "kipaumbele" chake kilikuwa kujiunga na Sevilla kwa mkopo kutoka Manchester United. ***(Diario de Sevilla,via Mail)***

### AKANJI ANUKIA UNITED

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick ana nia ya kumsajili mlinzi wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Uswisi, Manuel Akanji mwenye umri wa miaka 26. ***(Sport1,via Teamtalk)***

### NYOTA AIKATAA UNITED

GOLIKIPA wa Newcastle United, Martin Dubravka mwenye umri wa miaka 33, alikataa kuhamia Manchester United kwa mkopo katika dirisha la Januari. ***(Manchester Evening News)***

### ERIKSEN KUREJEA ARSENAL

TOTTENHAM Hotspur wanaweza kumrejesha, Christian Eriksen katika klabu hiyo kutoka Brentford baada ya kiungo huyo wa kati wa Denmark mwenye umri wa miaka 29 kukamilisha mkataba wake wa miezi sita. (Guardian)

### ARSENAL YAMBANIA ELNENY

ARSENAL ilikataa ofa katika dirisha la usajili la Januari kwa kiungo wa kati wa Misri, Mohamed Elneny kutoka Newcastle, Leeds na Watford, licha ya kwamba mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 unaelekea mwisho. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# WACHEZAJI MAN UNITED WAMTAKA POCHETTINO

●●● Ni baada ya hatima ya kocha huyo ndani ya PSG kutoeleweka huku...

**MANCHESTER, ENGLAND**

MAURICIO Pochettino amebakia mwenye nafasi kubwa zaidi ya kurithi mikoba ya Ole Gunnar Solskjaer kama kocha wa kudumu wa Manchester United, kwa mujibu wa gazeti la The Express.

Wachezaji wa kikosi cha kwanza cha Mashetani Wekundu hao wameweka wazi Pochettino ndiye wanayemhitaji hapo Old Trafford.

Kocha huyo raia wa Argentina amekuwa katika presha kubwa huko Paris Saint-Germain, kutokana na timu yake kutokuwa kwenye kiwango bora.

**Licha ya PSG kusheheni wachezaji wa kiwango cha dunia, kocha huyo amekuwa akishutumiwa anashindwa kupanga kikosi cha ushindi.**

Na kwa mujibu wa ripoti hiyo, wachezaji wa Manchester United wanaona Pochettino ni mrithi sahihi wa Solskjaer ambaye alitimuliwa kutokana na mwenendo mbaya wa timu.

Ralf Rangnick alipewa jukumu la kuwa kocha wa muda hadi mwishoni mwa msimu huu, lakini amekuwa akipata matokeo ya kuchanganya na hivyo kufanya uwezekano wa kupewa kazi hiyo kwa mkataba wa kudumu kupotea.

Majina kadhaa makubwa ya makocha Ulaya yamekuwa yakitajwa pia kuwania nafasi hiyo ya kuinoa United.

Kocha wa Ajax, Erik Ten Hag naye ni mmoja wa makocha wanaotajwa sana kuwania nafasi hiyo.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 918

MECHI KALI
PARIS ST GERMAIN
VERSUS
RENNES
1 | 1.62
X | 4.07
2 | 4.93

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# ARTETA AELEZA SABABU KUMUUZA AUBAMEYANG

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema "suluhu, siyo tatizo" katika uhusiano wake na mshambuliaji wa zamani wa washikabunduki hao, Pierre-Emerick Aubameyang.

Aubameyang, mwenye umri wa miaka 32, alivuliwa unahodha huo baada ya "makosa ya kinidhamu" Desemba, mwaka jana.

Mshambuliaji huyo alisema "lilikuwa ni tatizo tu na (Arteta)", wakati alipojiunga na Barcelona kwa uhamisho huru wiki iliyopita.

Arteta alijibu Jumatano, akisema: "Ilikuwa ni suluhu kwa asilimia 100. Ninaweza kutazama machoni mwa kila mtu."

"Ninafanya mambo mengi kimakosa, kusema kweli lengo kila wakati ni bora na sio kwangu mimi, ni kwa ajili ya timu nzima.

"Ninashukuru sana kwa kile Auba alichokifanya katika klabu na mchango wake tangu alipokuwa hapa. Jinsi ninavyojitazama mimi katika uhusiano ule ni suluhu, siyo tatizo."

Arteta alithibitisha kuwa mshambuliaji Mfaransa Alexandre Lacazette atakuwa nahodha wa Arsenal hadi mwishoni wa msimu, wakati ambapo mkataba wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 30 utakapokaribia kumalizika.

Alipoulizwa kuhusu mchezaji wa kimataifa wa Gabon, Aubameyang kusema yeye alikuwa tatizo. Raia huyo wa Hispania alisema: "Hayo ni maoni yake, hilo ndilo alililosema na unapaswa kuheshimu hilo.

"Iliishia kuwa njia bora iliyowezekana kwa kila mmoja, ninadhani wakati mambo yalipobadilika, na dhana ilibadilika, hii ni sehemu ya soka," alisema Arteta.


# Mourinho amchana Sanchez

**ROME,** Italia

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, ameamua kufunguka kwa nini Alexis Sanchez alikuwa hana mwendelezo mzuri wa kiwango chake alipokuwa anakipiga kwenye klabu ya Manchester United.

Sanchez alisajiliwa kutoka Arsenal katika usajili uliohusisha mabadilishano ya mchezaji na kiasi cha fedha.

Lakini hakuweza kuwa katika kiwango bora akiwa chini ya Mourinho na kuamua kumtoa kwa mkopo kwenda Italia Inter Milan.



Sanchez tangu apelekwe kwa mkopo Inter na baadaye kusajiliwa jumla, hajawa na mwendelezo mzuri wa kiwango chake na katika mchezo ambao Inter walishinda mabao 2-0 dhidi ya Roma ndipo waandishi walipopata nafasi ya kuuliza nini kilimsibu akiwa chini yake kwa kutokuwa na kiwango kizuri.

Mourinho alisema, "Nilizungumza naye kidogo kabla ya mchezo kuanza, tukiwa bado Uingereza hakuwa vizuri kule.

"Wakati yupo hapa Inter, anafuraha na amefunga bao bora ambalo limebadilisha mchezo.

"Lakini ukweli ni kwamba, kule Manchester United hakuwa na uwezo huo na ndio maana akaondoka."

## HABARI MICHEZO

,137,180

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/02/22 | 18:00 | Brentford vs Crystal Palace | 2.60 | 3.09 | 2.84 |
| 02. 12/02/22 | 18:00 | Peterborough vs Preston | 2.75 | 3.15 | 2.51 |
| 03. 12/02/22 | 18:00 | Reading vs Coventry | 2.79 | 3.19 | 2.45 |
| 04. 12/02/22 | 18:00 | Birmingham vs Luton Town | 2.81 | 3.15 | 2.46 |
| 05. 12/02/22 | 18:00 | Nottingham vs Stoke City | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 06. 12/02/22 | 18:15 | Villarreal vs Real Madrid | 2.74 | 3.32 | 2.54 |
| 07. 12/02/22 | 18:15 | Perugia vs Frosinone | 2.40 | 3.14 | 2.90 |
| 08. 12/02/22 | 20:00 | Napoli vs Inter | 2.81 | 3.41 | 2.44 |
| 09. 13/02/22 | 15:00 | Sheffield Wed vs Rotherham | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 10. 13/02/22 | 16:00 | Alaves vs Valencia | 3.04 | 3.24 | 2.36 |
| 11. 13/02/22 | 18:00 | Real Oviedo vs Huesca | 2.46 | 3.15 | 2.81 |
| 12. 13/02/22 | 19:00 | Kasimpasa vs Alanyaspor | 2.61 | 3.30 | 2.56 |
| 13. 13/02/22 | 19:30 | Leicester vs West Ham | 2.85 | 3.45 | 2.38 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 11/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4550 | Express FC vs Tooro United | 1.07 | 8.11 | 23.16 |
| 15:30 | 5708 | Nomme Kalju vs HJK Helsinki | 4.00 | 5.40 | 1.60 |
| 16:00 | 1025 | SC Kfar Qasem vs Hapoel Acre | 2.08 | 3.10 | 3.90 |
| 16:00 | 1809 | Sectzya Nes Ziona vs Hapoel Rishon Lezion | 2.16 | 3.06 | 3.56 |
| 16:00 | 2507 | SC Villa vs Bright Stars | 2.16 | 3.15 | 3.60 |
| 16:00 | 4103 | Hapoel Afula vs Bnei Yehuda | 4.55 | 3.46 | 1.78 |
| 16:00 | 4630 | AS Ashdod vs Hapoel Kfar Saba | 3.05 | 2.90 | 2.60 |
| 16:00 | 4830 | Ahi Nazareth vs Hapoel Ramat Gan | 2.24 | 3.00 | 3.60 |
| 16:00 | 5165 | El Fahem vs Beitar Tel Aviv Ramla | 1.94 | 3.20 | 4.30 |
| 16:00 | 5256 | Inter Turku vs IFK Mariehamn | 1.52 | 3.80 | 5.58 |
| 16:00 | 5687 | Altinordu vs Genclerbirligi | 2.50 | 3.26 | 2.54 |
| 16:00 | 5956 | Mekelakeya vs Welayta Dicha FC | 2.75 | 2.84 | 2.60 |
| 16:05 | 5647 | Abha vs AL Hazm | 1.75 | 3.66 | 4.45 |
| 16:30 | 3372 | PSS Sleman vs Persib Bandung | 5.38 | 3.13 | 1.68 |
| 17:00 | 3528 | Bengaluru FC vs Hyderabad FC | 1.72 | 3.95 | 3.75 |
| 17:30 | 3353 | PSM Makassar vs Pusamania Borneo | 2.45 | 2.89 | 2.89 |
| 18:10 | 3284 | Al Fateh (KSA) vs Al Ahli Jeddah | 2.14 | 3.42 | 3.22 |
| 19:00 | 1213 | Ajman Club vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 3.22 | 3.41 | 2.02 |
| 19:00 | 1966 | Stellenbosch vs Baroka FC | 1.88 | 2.95 | 4.35 |
| 19:00 | 4276 | Arba Minch Kenema vs Dire Dawa Kenema FC | 2.37 | 2.75 | 3.18 |
| 19:00 | 4581 | Samsunspor vs Bursaspor | 1.53 | 3.94 | 5.19 |
| 19:00 | 5777 | Zemplin Michalovce vs SKF Sered | 1.99 | 3.42 | 3.28 |
| 20:00 | 3012 | Gornik Leczna vs Slask Wroclaw | 2.51 | 3.14 | 2.61 |
| 20:00 | 4286 | Altay vs Caykur Rizespor | 2.05 | 3.31 | 3.50 |
| 20:00 | 5800 | HNK Sibenik vs Hrvatski Dragovoljac | 1.48 | 4.12 | 5.56 |
| 20:20 | 2918 | Al Ittihad Jeddah vs Al Nasr Riyadh | 2.26 | 3.50 | 3.00 |
| 20:55 | 2747 | Rapid Bucuresti vs Sepsi Osk | 2.71 | 2.86 | 2.76 |
| 21:30 | 4126 | Rapid Vienna vs RB Salzburg | 5.03 | 4.26 | 1.50 |
| 22:00 | 1306 | FC Volendam vs Jong AZ Alkmaar | 1.31 | 5.29 | 7.45 |
| 22:00 | 1659 | Heracles Almelo vs Utrecht | 2.99 | 3.33 | 2.24 |
| 22:00 | 3410 | De Graafschap vs Dordrecht | 1.35 | 5.05 | 6.80 |
| 22:00 | 3622 | Ujpest FC vs Kisvarda FC | 2.75 | 3.33 | 2.30 |
| 22:00 | 4100 | FC Oss vs FC Eindhoven | 2.74 | 3.37 | 2.36 |
| 22:00 | 4453 | RS Waasland Beveren vs KFC Oosterzonen | 1.85 | 3.81 | 3.56 |
| 22:00 | 4647 | Helmond Sport vs Telstar | 3.12 | 3.37 | 2.14 |
| 22:00 | 4904 | Almere City vs Emmen | 3.37 | 3.52 | 1.98 |
| 22:00 | 5418 | ADO Den Haag vs Maastricht | 1.27 | 5.48 | 8.61 |
| 22:00 | 5490 | SBV Excelsior vs Jong Ajax | 2.48 | 3.50 | 2.53 |
| 22:15 | 2242 | FC Schaffhausen vs FC Vaduz | 2.45 | 3.42 | 2.50 |
| 22:30 | 3720 | Cracovia vs Lechia Gdansk | 2.60 | 3.23 | 2.46 |
| 22:30 | 5501 | RB Leipzig vs FC Koln | 1.45 | 4.86 | 5.95 |
| 22:45 | 1683 | Glentoran Belfast vs Linfield Belfast | 2.57 | 3.25 | 2.48 |
| 22:45 | 2740 | Edinburgh City vs Stirling | 2.08 | 3.38 | 3.09 |
| 22:45 | 5252 | RFC Seraing vs Royal Antwerp | 3.74 | 3.74 | 1.85 |
| 23:00 | 1453 | Sevilla FC vs Elche | 1.42 | 4.40 | 7.80 |
| 23:00 | 1919 | Shamrock Rovers vs St Patricks | 1.83 | 3.42 | 3.81 |
| 23:00 | 3882 | Paris St Germain vs Rennes | 1.62 | 4.07 | 4.93 |
| 23:00 | 4676 | Arsenal Sarandi vs Rosario Central | 3.82 | 3.28 | 1.87 |
| 23:00 | 5358 | Leganes vs Zaragoza | 2.18 | 3.04 | 3.43 |
| 23:15 | 2967 | Porto vs Sporting Lisbon | 2.00 | 3.40 | 3.55 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Mmarekani wa Azam kuwapa nafasi vijana

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Abdilhamid Moallin, amesema moja ya mipango yake ndani ya timu hiyo ni kuwapa kipaumbele wachezaji vijana ambao wanatoka katika kituo chao ili kushiriki kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea hapa nchini.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Moallin, alisema anataka atakapoondoka Tanzania akumbukwe kwa kuwaendeleza wachezaji vijana ambao wamekulia kwenye kituo hicho.

Moallin alisema tayari matunda ya uamuzi wake yameanza kuonekana kwa mchezaji, Tepsie Evans na wenzake kwa kuisaidia timu kubwa kusaka matokeo chanya kwenye ligi.

"Hii inaonyesha kituo kimefanikiwa katika uendelezaji wa wachezaji, kwanini tusiwape nafasi, kutokana na uwezo wa Tepsi na wengine tunaendelea kuwatumia pia, na sasa tunatafuta mwingine kutoka kituo cha vijana kumpa nafasi katika kikosi cha timu ya wakubwa," alisema Moallin.

Aliongeza uwezo wa wachezaji vijana umemshawishi kuwatumia na anaamini anawafurahisha makocha wa timu za vijana kwa kuwaamini nyota waliowakuza.

"Tunahitaji kuwaamini vijana na kuwapa nafasi ya kuonyesha, kwa sababu jambo hilo halihitaji vitu vingi kwa sababu wachezaji wote vijana wanapata mafunzo mazuri na kuleta matumaini makubwa," Moallin alisema.

Aliongeza kitendo cha klabu kumiliki kituo ni jambo sahihi katika maendeleo ya soka na Azam FC tayari ni wazalishaji wakubwa wa nyota chipukizi na matunda yake yanaonekana katika timu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Moallin alisema amevutiwa sana na sera ya uendeshaji ya wachezaji wa Azam na ataitumia sera hiyo kuhakikisha wachezaji wanaokulia katika kituo hicho wanafika katika ngazi za juu za ubora wa soka na baadaye kuwa fahari ya klabu.

# FUNDI SELEMALA ASHINDA JACKPOT




**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Mbezi Beach Africana, jijini Dar es Salaam, John Bugenyi, ameshinda Sh. milioni 4.7 katika Jackpot Bonus ya SportPesa iliyochezwa mwishoni mwa wiki iliyoisha, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 11.

Akizungumza baada ya makabidhiano ya mfano wa hundi katika ofisi za Sportpesa jijini, John alisema alianza kucheza na Sportpesa miaka kadhaa iliyopita. "Nilianza kucheza na Sportpesa kama sikosei miaka minne iliyopita".

Kwa mujibu wake, John ambaye pia ni fundi selemala, alisema alivutiwa sana na jina la SportPesa, kabla ya rafiki yake mmoja kumtambulisha rasmi kwa kumuelekeza namna ya kucheza.

"Ujue nina rafiki yangu mkubwa sana anayeitwa Maganga, yeye alikutana na mimi na kunionyesha namna ya kujisajili na kucheza. Na baada ya hapo niliweza kucheza mwenyewe," alisema John.

Mimi katika michezo ya kubashiri ya Sportpesa nacheza aina moja tu ya mchezo ambao ni Jackpot. Na katika jambo hili la ubashiri sina utani wala maskhara hata kidogo. "

Huwa nacheza Jackpot tu. Na kwa siku ambapo Jackpot inatoka huwa nacheza mikeka kama saba au nane.

Akielezea namna alivyopata ushindi huu wa Jackpot bonus anasema aliona mkeka wa jackpot siku ya Jumatatu na kuanza kucheza papo hapo. "Sikusubiria cha Ijumaa wala cha Jumamosi, nilichagua timu zangu ninazoziamini muda ule ule nilipoziona timu, na baada ya hapo sikuzifuatilia".

# Michezo

Ijumaa Februari 11, 2022

Nipashe




Mourinho amchana Sanchez UKURASA 22

# SIMBA: TUTAWAPA RAHA WATANZANIA

## ●●●Yatamba na One Team, One Dream huku Asec Mimosas ikiwasili...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inaanza vyema hatua ya makundi katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia kwenye michuano ya kimataifa, Simba imetambulisha rasmi kauli mbiu itakayochochea ushindi iitwayo 'One Team One Dream, Simba Nguvu Moja'.

Simba itawakaribisha Asec Mimosas katika mchezo wa kwanza wa Kundi D utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Wekundu wa Msimbazi watashuka dimbani katika mchezo huo huku wakitangaza vivutio vya utalii kwa kuvaa jezi zenye nembo ya Visit Tanzania ikiwa ni mara ya pili baada ya kufanya hivyo pia msimu uliopita katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).**

Akizungumza jijini jana Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema kutokana na heshima iliyonayo Simba na michuano hiyo mikubwa, wamepanga kuitangaza nchi kivingine kupitia sekta ya utalii.

"Nilipokuwa nchini Cameroon nilipopata mwaliko kule, timu yetu ni tofauti na huku tunavyoiona Simba ni timu kubwa sana, katika takwimu za timu zinazofuatiliwa zaidi ni namba moja," alisema Barbara.

Ofisa huyo alisema wameendelea kukiimarisha kikosi hicho na malengo ya Simba msimu huu ni kutwaa Kombe la Ligi Kuu na kutetea Kombe la FA, lakini kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii, Jaji Mstaafu, Thomas Mihayo, alisema Simba ni mabalozi wakubwa wa utalii ambao wanaufanya kupitia jezi wanazovaa katika michuano hiyo na uamuzi huo umesaidia kuongeza idadi ya watalii wa ndani na nje.

"Kupitia Visit Tanzania Watanzania wengi mwaka uliopita wamepata mwamko wa kutembelea vitutio, baadhi ya hoteli kwenye vivutio vya utalii zilikuwa zimejaa na asilimia 90 walikuwa Watanzania,"

"Hata watalii wa nje pia wanakuja hapa nchini kuangalia Simba ni nani na wana utamaduni gani, nawaomba Watanzania waendelee kutembelea vituo vya utalii," alisema Mihayo.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Simba, Ahmed Ally, alisema maandalizi ya mchezo huo kwa upande wa uongozi yamekamilika na kilichobaki wamemwachia kocha Pablo Franco kumalizia kazi yake.

"Huu ni mchezo mkubwa zaidi Afrika na kuona hilo Rais wa heshima wa Simba, Mohamed Dewji 'Mo', ametoa zawadi kwa mashabiki kwa kutoa punguzo la bei ya tiketi za mzunguko kutoka Sh. 5,000 hadi Sh. 3,000.

" Hii kwa ajili ya kuongeza motisha kwa mashabiki na msimu huu tunaingia na kauli mbiu ya 'One Team One Dream' ambayo tulianza nayo siku ya Simba Day na ndio itakuwa kauli mbiu yetu ya msimu," alisema Ally.

Alisema anaamini wachezaji wa Simba watapambana kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo muhimu na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele.

"Sisi tumekabidhiwa jukumu la kuwapa raha Watanzania, tutafanya hivyo In Shaa Allah," Ally alisema.

Naye Beki Shomari Kapombe, amesema kikosi chao kimeendelea na mazoezi kwa ajili ya kuhakikisha wanaanza vyema hatua hiyo ya makundi.

"Kila mchezaji anajua umuhimu wa mchezo huo, tunajua umuhimu wa mchezo huo ili kujiweka vizuri katika msimamo wa kundi letu, ninaimani tutafanya vizuri, tunahitaji pointi tatu," alisema Kapombe.

Wakati huo huo, kikosi cha Asec Mimosas kiliwasili nchini jana mchana tayari kwa mchezo huo wa kwanza utakaochezwa kuanzia saa 10:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki.




Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Jaji mstaafu Thomas Mihayo (katikati), akiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez (kushoto) na Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, wakionyesha jezi za timu yao zilizozinduliwa kwa ajili ya kutumika kwenye mechi za hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kibano wasanii wanaochafuana

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, imesema imebaini limeibuka wimbi kubwa la wasanii kuchafua wenzao.

Aidha, limesema ipo haja kwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, kuchukua hatua kwa kuhakikisha maadili ya wasanii yanazingatia hadhi ya tasnia ya filamu na muziki nchini.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, akiwasilisha maoni ya kamati hiyo bungeni jana, alisema walibaini changamoto nyingi katika ukuaji wa tasnia hiyo ikiwamo ushirikiano mdogo unaotolewa wa waandaji wa filamu na wasanii wanaopeleka muziki nje ya nchi.

Aidha, alisema ni muhimu serikali kuweka mkakati kukamatwa maharamia wa kazi za wasanii ili wachukuliwe hatua na wasanii hao wanufaike na kazi zao.

Nyongo alisema ni muhimu pia ukawepo mkakati kuhakikisha "script" za filamu zinakuwa katika lugha fasaha, ili kuvuta soko la ndani na nje, pamoja na uandaaji wa filamu kuwa na uhalisia ili kuvutia watazamaji.

"Nchi nyingi ikiwamo India zimenufaika kiuchumi, kisiasa na kijamii kupitia tasnia ya filamu. Nchi yetu bado hatujanufaika ipasavyo kutokana na changamoto mbalimbali zinazoikumba tasnia hii," alisema.

9 770856 541002 >